Jumatatu Aprili 22, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581654
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




UKURASA 11

**Waandishi** wa IPP wang'ara tuzo kimataifa elimu ya afya

UKURASA 3



**Samia** amlilia Gardner Habash, kuzikwa kijijini kwao Kikelelwa

UKURASA 5



**ACT** Wazalendo yataka Muungano unufaishe pande 2

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipunga mkono kuwaaga viongozi wa dini waliosafiri kwa treni ya mwendokasi (SGR) safari ya kwanza ya majaribio kutoka Stesheni ya Dar es Salaam kwenda jijini Dodoma jana, ambako watashiriki katika maombi maalum ya kuliombea Taifa. **PICHA: OWM**

## SGR yaanza rasmi Safari majaribio Dar kwenda Dodoma

UKURASA 19

# Makonda aitwa Kamati ya Maadili CCM



• **Kuhojiwa** leo, mwenyewe asema... *Uk. 2*



Joseph Mbilinyi



Mchungaji Peter Msigwa

UCHAGUZI CHADEMA

## Sugu, Msigwa mchuano mkali

UKURASA 3




**MICHEZO** SIMBA, YANGA REKODI ZATAWALA DABI UK.24
**MAONI,** UK.6

# Makonda kuhojiwa Kamati ya Maadili CCM

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, leo anatarajia kuhojiwa na Kamati ya Maadili ya Chama cha Mapinduzi (CCM) jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa chanzo cha kuaminika ndani ya chama hicho, kuna uwezekano mkubwa Makonda akahojiwa na kamati hiyo baada ya kupewa barua ya kuitwa tangu Jumamosi iliyopita.

Aidha, chanzo chetu kilidokeza kuwa Makonda anatarajiwa kama ilivyopangwa kuhojiwa leo majira ya saa nne asubuhi ofisi za Makoa Makuu ya chama mkoani Dodoma na kamati hiyo ambayo inaongozwa na Mwenyekiti wake ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Kanali mstaafu, Abdulrahman Kinana.

Chanzo hicho kilidokeza kuwa inawezekana Makonda katika kikao hicho akahojiwa kutokana na kauli anazozitoa ambazo zinakwenda kinyume na matakwa ya chama hicho.

Hata hivyo, chanzo hicho hakikufafanua zaidi kuhusu agenda za kikao hicho na kama kuna tuhuma zozote zinazomkabili Mkuu huyo wa Mkoa wa Arusha, ambaye alianza kutumikia mkoa huo katika siku za karibuni baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Hata hivyo, wakati wa maadhimisho ya miaka 40 ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Sokoine, Mkuu huyo wa mkoa, alipokuwa akiwasilisha salamu za mkoa wake, alidai kuwapo kwa viongozi wakiwamo baadhi ya mawaziri wanaolipa fedha watu kumtukana Rais Samia kwenye mitandao ya kijamii.

Gazeti hili lilipomtafuta Makonda kuhusu wito huo, hakuthibitisha wala kukanusha.

Majukumu ya Kamati ya Maadili ya CCM ni kupokea taarifa za wanachama na viongozi wanaotuhumiwa kukiuka kanuni, taratibu na maadili kichama na kuzifanyia uchunguzi.

Kazi ya Kamati hiyo ni kuchunguza tuhuma za wanachama na viongozi kupendekeza adhabu au hatua za kuwachukulia wanachama na viongozi ambao wanakiuka maadili, wanaokwenda kinyume cha Katiba ya chama, miongozo na kanuni.

Pia kufuatilia mienendo ya viongozi na wanachama wanaotuhumiwa kukiuka taratibu.

Katika kipindi cha uchaguzi kamati hiyo huchunguza mienendo ya wanachama ambao wanawania nafasi za uongozi na kutoa taarifa kwenye Sekretarieti, Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao.



Balozi wa Urusi nchini, Andrey Avetisyan (kushoto), akibadilishana mawazo na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Azania Front, Charles Mzinga baada ya kuzindua maonyesho ya picha kuhusu maisha ya Yesu zilizochorwa na mchoraji maarufu wa Urusi, Vasily Polenov katika karne ya 19, katika usharika huo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwigulu aishukuru WB kuidhinisha trilioni 9/- kutekeleza miradi 14

**Na Benny Mwaipaja, WASHINGTON D.C**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameishukuru Benki ya Dunia (WB) kwa kuidhinishia Tanzania miradi 14 ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya dola za Marekani bilioni 3.87 (sawa na Sh. trilioni 9.9), kupitia mpango wa benki hiyo wa utoaji mikopo na misaada (IDA-20).

Fedha hizo zimeelekezwa katika miradi ya sekta za elimu, afya, hifadhi ya mazingira, miundombinu, nishati na Tanzania ya Kidigiti.

Dk. Nchemba alitoa shukrani hizo wakati akizungumza na Makamu wa Rais wa WB, anayesimamia nchi za Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Victoria Kwakwa, wakati wa Mikutano ya Kipupwe (Spring Meetings) ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), jijini Washington DC, Marekani.

Alisema miradi hiyo 14 ni kati ya miradi 25 ya kimkakati yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 5, ambayo serikali iliiwasilisha kwenye benki hiyo kwa ajili ya kupatiwa fedha, ili iweze kutekelezwa na kuchangia kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi, maendeleo ya nchi na kupunguza umasikini kupitia malengo yaliyowekwa katika Dira ya Taifa ya 2025.

Dk. Nchemba aliishukuru pia benki hiyo kwa kutoa awamu ya kwanza ya kiasi cha dola za Marekani milioni 500 kati ya kiasi cha dola milioni 750, mwezi Desemba mwaka 2023, kwa ajili ya kuchangia bajeti ya serikali, ili kukabiliana na athari za UVIKO-19 na vita vinavyoendelea baina ya Ukraine na Urusi kwa kuwekeza kwenye miradi inayochochea uchumi na huduma za jamii.

Aidha, Dk. Nchemba aliishukuru WB kwa kuahidi kusaidia ujenzi wa mradi wa Kikanda wa Reli ya Kisasa (SGR) utakaoziunganisha nchi za Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, mradi ambao ni muhimu kwa ajili ya kuchochea biashara, ukuaji wa uchumi, kuboresha mtandao wa miundombinu ya usafiri na usarishaji, kudhibiti mabadiliko ya tabianchi na kukuza ajira katika ukanda huo.

Akizungumza katika Mkutano huo, Makamu wa Rais wa WB anayezisimamia nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika, Victoria aliipongeza Tanzania kwa hatua mbalimbali inazozichukua katika kusimamia uchumi na maendeleo ya wananchi wake na kwamba mafanikio hayo yanapaswa kuigwa na nchi nyingine.

Aliahidi kuwa WB iko tayari kuendelea kusaidia Tanzania ili iweze kufikia malengo yake ya maendeleo kwa kuipatia fedha na utaalam kwa kuziwezesha sekta muhimu za uzalishaji na huduma za jamii kushamiri kikiwemo kilimo, nishati, uchumi wa kidigiti, hifadhi ya mazingira, maji, elimu na ujenzi wa wa miundombinu ya usafirishaji.

Aidha, Kwakwa aliahidi pia kuwa WB itashiriki kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR ya kikanda itakayotekelezwa katika nchi tatu za Tanzania, Burundi na DRC kwa kuwa mradi huo ni muhimu katika kukuza biashara na uwekezaji katika Ukanda mzima wa nchi za Afrika.

# ACT Wazalendo yataka Muungano unufaishe pande zote

**Na Rahma Suleiman**

MWENYEKITI wa ACT-Wazalendo Taifa, Othman Massoud Othuman, amesema kuna umuhimu wa vijana kuendeleza harakati za amani, kudai Muungano wenye manufaa kwa pande zote za Tanzania Bara na Zanzibar.

Kiongozi huyo aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha mada katika kongamano la vijana lililoshirikisha wanachama na wasomi wa vyuo vikuu, ikiwa ni kuelekea maadhimisho ya miaka 10 ya kuzaliwa kwa chama hicho, Mei 5.

Alisema kwa muda mrefu tangu Zanzibar iungane na Tanganyika mwaka 1964, haijawahi kunufaika na usawa kwenye Muungano huo, ambao kwa mara kadhaa umekua ukilalamikiwa na kuundiwa tume bila ya mafanikio yoyote.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, alisema kwa mfumo ulipo sasa wa Muungano, kuna haja kubadilishwa kwa sababu hautoi haki sawa kwa pande zote mbili za washiriki, isipokuwa unaupa faida upande mmoja.

Aidha, alisema kwa muda wote tangu kuasisiwa Muungano huo, umekua ukifanya kazi zaidi ya kuidhibiti Zanzibar kila sekta na ndio maana mambo muhimu ambayo yanaendeleza nchi yamebaki kuwa mambo ya Muungano.

Alitaja miongoni mwa mambo hayo na kusema ni umuliki wa Benk Kuu, ambayo ina kazi ya kusimamia sarafu ya nchi na utambulisho nje ya mipaka ya Tanzania.

" Hata kuundwa kwake hiyo Benki kuu Tanzani (BoT) sehemu ya mtaji ambao ulioanzisha kuna asilimia ya fedha ambayo ilitoka Zanzibar, baada ya kuvunjika kwa bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki ambayo ilikua mwanachama," alisema.

Pamoja na hayo alisema wataendelea kudai haki ya Zanzibar katika benki hiyo kwa sabababu wanao ushahidi wa kutosha wa kuwapo kwa asilimia iliyotoka Zanzibar.

Akizungumzia changamoto nyingine, alisema Muungano ni suala zima la mafuta na gesi ambalo nalo lilingizwa kwenye mambo ya Muungano bila ya makubaliano yoyote ya pande husika.

Kwa mujibu wa Othman, bahati mbaya baadhi ya watu ambao wana nafasi za juu, serikalini upande wa Zanzibar wanaendelea kuamini kuwa wana mamlaka ya kuchimba mafuta na gesi kisheria iwapo yatabainika uwapo wake, wakati jambo hilo halina ukweli na linabanwa na sheria ya Muungano.

Awali, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Ismail Jussa, alisema Zanzibar kwa muda wote ambao imeungana na Tanzania Bara, imepoteza fursa muhimu ambazo kama zingewekwa sawa ingepiga hatua zaidi za kimaendeleo.

Alisema Zanzibar inahitaji aina ya Muungano wa nchi mbili huru ambao utatoa fursa sawa kwa washiriki wote na sio upande mmoja kunufaika zaidi kuliko mwingine.

Makamu Katibu Mtendaji wa Ngome ya Vijana, taifa wa chama hicho, Mohamed Busara, alisema vijana wana wajibu wa kujitambua na kufahamu wanachokitaka.

Aidha, alisema kwa bahati mbaya vijana wa kizanzibar wamekua wakidanganywa na kupewa ajira, huku wakikataa na kuacha mambo muhimu kwa mustakbali wao na maisha yao.

# Sugu, Msigwa kivumbi na jasho kuwania uenyekiti

**Na Elizabeth Zaya**

NI 'kivumbi' cha watia nia kwenye nafasi ya Uenyekiti Kanda ya Nyasa kuelekea kwenye uchaguzi wa viongozi wa Kanda mbalimbali za Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), unaoendelea sasa.

Tofauti na ilivyo kwenye kanda mbalimbali za chama hicho ambazo zinatarajia kufanya uchaguzi huo Mei, mwaka huu, Kanda ya Nyasa inaonekana kuwa na ushindani mkali kuliko nyingine kutokana na wafuasi wa wagombea hao kuwa na mbwembwe nyingi ikiwamo majibizano kwenye mitandao ya kijamii kila upande ukionyesha na ushawishi wa kushinda.

'Vigogo'wawili' machachari wa chama hicho, Joseph Mbilinyi maarufu kama Sugu (pichani) na Peter Msigwa, ndio wanaotia nia ya kuwania nafasi hiyo, huku wafuasi wao wakiwa na sare zenye picha na maneno zikiwapigia debe wagombea wao.

Sugu anagombea kwa mara ya kwanza, lakini Msigwa anapambana kutetea nafasi hiyo kwa kuwa mpaka sasa ndiye mwenyekiti wa kanda hiyo.

Duru za siasa zinaeleza kuwa Sugu ndiye Mbunge aliyeshinda kwa kura nyingi uchaguzi mkuu wa 2015 kwa kupata kura 97,675 huku mpinzani wake akipata 46,894.

Wote kwa nyakati tofauti, walijinasibu kwamba wameamua kufanya hivyo kutokana na shinikizo la wafuasi wao ambao ndio wanachama na wapiga kura wao.

Jana vigogo hao kwa nyakati tofauti, walirejesha fomu huku kila upande ukionyesha mbwembwe kwa mamia ya wafuasi wao wanaowaunga mkono ambao waliwasindikiza kurejesha fomu hizo.

Msigwa akiwa na kundi kubwa la wafuasi wake alirejesha fomu kwa 'staili' akiwa amenyanyuliwa juu na wafuasi wake hao huku wakiimba nyimbo za dini.

Mmoja wa wafuasi wa Msigwa aliyekuwa akiongoza msafara wakati kiongozi wao akirudisha fomu hiyo, alisikika akisema wafuasi hao walitoka katika mikoa mitano ya kanda hiyo ambao pia ni wapiga kura.

Kadhalika, Sugu na kundi kubwa la wafuasi wake walimsindikiza na baada ya kurudisha fomu hiyo alisema ameamua kubeba jukumu hilo baada ya kusukumwa na wanachama waliotaka mabadiliko kwenye kanda hiyo.

"Kwa nafasi yangu, yale niliyoyafanya kwenye chama, rekodi ya kazi zangu huko nyuma, nikaona nitakuwa mbinafsi kama nitagoma juu ya heshima ambayo wenzangu mmenipa kwa sasa katika kuelekea uchaguzi huo, mmenipa heshima kubwa na mwanzo mliposema tuko pamoja nikajua ni utani maana mjini ukiambiwa tuko pamoja ukigeuka nyuma huoni mtu," alisema Sugu.

"Lakini kufikia jana (juzi), kwenye kikao chetu ambapo mlijikusanya kama viongozi na wapigakura na mkasema kwamba mje tuonane kuhakikisha kwamba mko pamoja na mimi, tena kutoka mikoa yote mitano, kwa kweli niliamini, kwa hiyo nawashukuru sana."

"Niko tayari kufanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa kwa sababu sijaianza leo, leo ni kurudisha fomu tu, kampeni hazijaanza, yale mengi yanayohusiana na kujieleza kwamba tutafanya nini nitakuja kuyaeleza kwenye maeneo yenu wakati utakapofika kwa sababu nitazunguka katika majimbo yote 31 katika mikoa mitano kuja kuzungumza na ninyi uelekeo wetu wa mbele ili kuakisi kiu



ya mabadiliko mnayoyataka katika Kanda ya Nyasa," alisema Sugu.

Aidha, alitaja vipaumbele vyake endapo atachaguliwa katika nafasi hiyo kuwa ni pamoja na kurejesha kanda hiyo kwa wanachama na siyo kujifungia ndani na kufanya uamuzi peke yake na kupuuzia maoni ya wanachama.

Kipaumbele cha pili alisema ni kwenda kusimamia makakati wa kusaka ushindi katika uchaguzi wa serikali za mitaa 2024 na uchaguzi mkuu 2025 pamoja na kusimamia programu ya 'CHADEMA Digital'.

Uchaguzi huo wa kanda unafanyika baada ya kumalizika wa wilaya na mikoa na baadae utatangazwa uchaguzi wa mwenyekiti taifa.

Wengine wanaotajwa kutia nia ya kuchuana katika uenyekiti katika kanda mbalimbali kwenye mabano ni Ezekiel Wenje, John Heche na John Pambalu (Kanda ya Victoria), Boniface Jacob na Baraka Mwago (Kanda ya Pwani), Gaston Shundo na Dickson Matata (Kanda ya Magharibi).

Aidha, Aisha Luja na David jumbe Kanda ya Kati wakati Kanda ya Kaskazini anayetajwa bado Godbless Lema pekee ambaye ndiye mwenyekiti.

# Wanahabari wanne IPP wang'ara tuzo afya kwa umma

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA Merck Foundation ambalo ni tawi la Merck KGaA Germany, kwa kushirikiana na wake wa Marais wa Barani Afrika, limewatangaza waandishi wa habari wa Tanzania 11, wanne kutoka Kampuni ya IPP washindi wa tuzo ya kimataifa elimu ya afya.

Tuzo hizo 'Merck Foundation Media Recognition Awards 2023', hutambua mchango wa vyombo vya habari katika kulinda utu wa mwanamke, msichana, jamii na elimu ya afya kwa umma, dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza (NCDs).

Waandishi wa IPP waliopata tuzo hizo ni Marco Maduhu, Shaban Njia na Christina Mwakangale (wote Nipashe), na Beatrice Philemon (The Guardian).

Wengine ni Aveline Kitomary (Habari Leo), Veronica Mrema (matukio na maisha blog), Adam Hando (CG Fm), Tulinagwe Malopa (Gazetini), Lucy John Bosco (Mwananchi), Mwanaisha Makumbuli (Highlands Fm) na Olga Lungala (Moshi Fm).

Maduhu, ametuzwa ushindi wa kwanza tuzo ya 'More Than a Mother', kipengele kinacholinda utu wa msichana, mwanamke na kuvunja unyanyapaa dhidi ya hali zao kiafya na kijinsia na Njia, akishika nafasi ya pili kwenye kipengele hicho.

Christina, alishika nafasi ya kwanza katika kipengele kinachotambua uandishi wa habari za afya dhidi ya NCDs, huku Beatrice akishika nafasi ya tatu kipengele cha wanawake kiuchumi na kulinda utu wao.

Shirika hilo ambalo hutangaza tuzo hizo kila mwaka, kutoa fursa kwa waandishi wa habari kutoka nchi za bara Afrika kushiriki, kutoka kanda mbalimbali ambazo ni; Kusini mwa Afrika; Afrika Mashariki na Afrika Magharibi na zinazozungumza lugha ya Kireno na Kifaransa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika hilo, Seneta Dk. Rasha Kelej, akitangaza majina ya washindi hao, kwenye mkutano uliowakutanisha washindi hao mwishoni mwa wiki, mtandaoni, alisema lengo la mashindano hayo ni kukuza uelewa, kutoa elimu husuan kwenye sekta ya afya, ili jamii iache unyanyapaa dhidi utasa, ugumba na kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema, washiriki wa tuzo hizo ni kutoka barani Afrika, walioshinda tuzo ya 'More Than a Mother' kupinga ukatili, kusaidia elimu ya msichana, kumwezesha mwanamke ni 53, huku tuzo ya 'Diabetes & Hypertension' ni 29.

Seneta Dk. Rasha, ambaye pia ni Rais wa Kampeni ya More Than a Mother', alisema: "Ninaona furaha kuwatangaza washindi wa Merck Foundation mwaka 2023, ambao wamekuwa ni sauti ya wasio na sauti."

"Washindi wa tuzo hizi wana mchango mkubwa kwenye kuelimisha umma, kuhusu ugonjwa wa presha na kisukari, ili kubadili mtindo wa maisha pia katika kupiga vita unyanyapaa dhidi ya ugumba, umuhimu wa elimu ya msichana, kuwezesha wanawake,

"Washindi wote watakabidhiwa tuzo ikiwamo fedha, medali pamoja na cheti na ni mabalozi tayari pia tunawakaribisha wengine wote kushiriki na kutuma maombi ya kuwania tuzo hizo za mwaka 2024," alisema Dk. Rasha.

# CRDB kuwekeza uanzishwaji Benki ya Taifa ya Ushirika

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

IKIWA imebaki miezi miwili kabla Rais Samia Suluhu Hassan hajaizindua Benki ya Taifa ya Ushirika Tanzania (CBT), Benki ya CRDB imeiomba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuangalia namna ya kuiongezea nafasi ya kuwekeza zaidi katika benki hiyo mpya inayotarajiwa kuhudumia zaidi wakulima hasa waliopo kwenye vyama vya ushirika.

Ombi hilo limetolewa na Mwenyekiti wa Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mariamu Mzuzuri aliyeongoza wajumbe wa kamati hiyo kupata taarifa za maendeleo ya mchakato ulioanza tangu mwaka 2012 wa kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika. Dk. Laay alisema kila kitu kinakwenda vyema kuiruhusu taasisi hiyo mpya ya fedha ianze kuhudumia Watanzania.

"Idadi ya Watanzania wanaotumia huduma za benki ni ndogo sana nchini. Ripoti ya Finscope 2023 inaonesha ni asilimia 22 tu. Lakini sote tunafahamu hapa kwamba uchumi wa taifa letu kwa kiasi kikubwa unategema kilimo, lakini wakulima wengi ndio hawana akaunti kwa sababu wanaishi vijijini," alisema Dk. Laay.

Benki ya CRDB ilishatoa Sh. bilioni saba ili kuinusuru Benki ya KCBL isife baada ya mtaji wake kuyumba na baada ya uwekezaji huo wa kimkakati, tayari zaidi ya Sh. bilioni 16.8 zimekusanywa ili kuanzisha benki mpya ya TCB.

Dk. Laay alitumia fursa hiyo kutoa ufafanuzi kuwa kwamba huko nyuma KCBL na Tacoba zilikuwa hazifanyi vizuri, hivyo serikali ikaiomba Benki ya CRDB iongeze mtaji kuziwezesha benki hizo.

"Fedha hizi zilitolewa si kama mkopo, bali sehemu ya umiliki kwani hisa za benki hii mpya zitakapoanza kuuzwa basi zitaingizwa kwenye ununuzi wa hisa hizo na kuongeza kiasi kingine ili kufikisha asilimia 20 ya hisa zote za benki hiyo.

Akiwakaribisha wajumbe wa kamati yake kuchangia mjadala wa kuanzishwa kwa benki hiyo mpya, Mzuzuri alipongeza maandalizi yaliyofanywa mpaka sasa na akasisistiza umakini zaidi kuhakikisha malengo yanatimia kama ilivyopangwa.

Akiwasilisha mpango wa kuanzishwa kwa benki hiyo, Meneja Mkuu wa Benki ya KCBL, Godfrey Ng'urah alisema inalenga kuongeza njia mbadala za mapato kwa vyama vya ushirika, kutoa huduma zenye gharama shindani kwa kuwafikia watu wengi zaidi, na kutoa bidhaa za fedha zinazokidhi mahitaji wanachama wa ushirika.

Kuhusu manufaa yake, alisema Benki hiyo ya Taifa ya Ushirika itagusa mnyororo mzima wa thamani kuanzia masoko ya bidhaa za wakulima kuanzia wanachama wa vyama vya msingi vya ushirika, wafanyabiashara wadogo, wafugaji, wavuvi na vikundi vya Vicoba pamoja na kufanikisha miradi ya kibiashara, uzalishaji, usafirishaji na ujenzi wa maghala na ununuzi wa pembejeo za kisasa.

Akieleza matumaini yaliyopo, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Benson Ndiege alisema licha ya mchakato huo kuchelewa kutekelezwa tangu pendekezo lilipotolewa mwaka 2012, kasi ya utekelezaji wake kwa sasa inakwenda vizuri.

"Tayari Tandahimba Community Bank imebadilishwa na kuwa Tandahimba Cooperative Bank (TCBL). Uzuri wa benki ya ushirika ni kwamba mteja ndiye mmiliki, hivyo inakuwa rahisi kwao kuilinda kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye," alisema Dk. Ndiege.

HABARI KITAIFA




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Deogratius Ndejembi, akizungumza wakati akifunga kikao kazi kati ya Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi, Kanda ya Kati ya Magharibi, Kamishna wa Kazi, Menejimenti ya Mfuko wa Fidia Kwa Wafanyakazi na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), mjini Kigoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaahidi ushirikiano kukuza tasnia ya habari

**Na Carlos Banda**

SERIKALI imeahidi kuboresha ushirikiano na vyombo vya habari nchini kuhakikisha wanahabari wanakuwa na uhuru wa kupata na kujieleza.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Msemaji wa Serikali, Mobhare Matinyi, wakati wa hafla ya uzinduzi wa bodi mpya ya Baraza la Habari Tanzania (MCT) iliyoambatana na kumuaga rasmi Katibu Mtendaji aliyemaliza muda wake, Kajubi Mukajanga, baada ya kuhudumu kwenye nafasi hiyo kwa miaka 15.

Kwa mujibu wa Matinyi, marekebisho ya sheria hiyo yamefanywa kwa ushirikiano na wadau ikiwamo MCT ili kuhakikisha kwamba wanahabari wanafurahia haki yao ya uhuru wa maoni na haki ya kupata habari na uhuru katika kazi zao za uhariri bila ya kuwa na uoga wa adhabu za kijinai.

Aidha, alisema marekebisho hayo yanalenga kuondoa wanahabari katika makosa yanayohusiana na kashfa za kijinai, makosa ambayo kwa kawaida yanaangukia katika utaratibu wa mashauri ya madai.

Matinyi ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, alisema marakebisho hayo yaliwaondolea adhabu wamiliki wa mitambo ya uchapishaji huku akibainisha kuwa kuondolewa kwa adhabu hiyo kulitokana na hoja kwamba kwa teknolojia ya sasa wamiliki hawana uwezo wa kudhibiti maudhui yanayochapishwa katika mitambo yao ya uchapishaji.

Aidha, alisema kuwa serikali ipo katika hatua za mwisho za uanzishwaji wa taasisi zilizo chini ya sheria ya huduma za habari sura namba 229 kwa lengo la kuendelea kukuza na kuimarisha sekta ya habari nchini na kuifanya ijisimamie yenyewe.

Matinyi alisemaa serikali inatambua changamoto zilizopo akirejea kuhusu uwapo wa kamati ya kuangalia changamoto za kiuchumi katika vyombo vya habari na kumbusha agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, kufanyia kazi na wataalam kutoka ndani ya sekta ya habari.

"Vyombo hivi vitakuwa ni Baraza Huru la Habari ambalo litakuwa na kamati ya malalamiko yenye mamlaka ya kimahakama, Bodi ya Ithibati ya Wanahabari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari," alisema.

Aidha, alimpongeza Katibu Mkuu mpya, Ernest Sungura akiamini utendaji wake utaleta mabadiliko kwenye sekta ya habari.

Katibu anayemaliza muda wake, Kajubi alisema matarajio yake kutoka kwa bodi mpya ni kufanya kazi kwa ushirikiano kwa lengo la kuleta mafanikio chanya na kusaidia kutatua changamoto zinazoletwa na ukuaji wa teknolojia katika tasnia ya habari ili kuhakikisha habari zinazotolewa kwa umma ni za kuaminika na zenye kuzingatia maadili.

"Naamini tupo na mafaniko zaidi katika usimamizi wa maadili na taalum. Utetezi wa mazingira bora zaidi ya waandishi kufanyia kazi, ushirikiano na serikali katika kukuza uhuru wa habari, ushirikiano na wadau wa ndani wa wakiwamo Coalition on the Right to Information (CORI) na wakikanda na kimataifa kama vile EAPC, na wengine pamoja na uongozi katika kukabiliana na changamoto mpya na katika kudaka fursa mpya zinazokuja na maendeleo ya kidijitali kama akili mnemba (AI) pamoja na mambo mengine," aliongeza.

Mwakilishi wa bodi inayomaliza muda wake, Edda Sanga, alisema kuwa jitihada nyingi zilielekezwa kuhakikisha wanahabari wanazingatia miiko na weledi kwenye taaluma uandishi wa habari na kuiona kuwa ni taaluma yenye heshima.

Aidha, alimpongeza Mukajanga kwa utayari aliokuwa nao kufanya kazi kwa uwazi na kwa kushirikiana na bodi na kuongeza kuwa katibu mtendaji huyo alijitahidi kuionyesha serikali kuwa vyombo vya habari si adui wa serikali bali walichohitaji wanahabari ni kuwa na ushirikiano na serikali ili kuleta maendeleo.

## Watatu mbaroni mauaji ya mwanafunzi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la polisi Mkoa wa Morogoro limewakamata watuhumiwa watatu kwa mauaji ya Makamu wa Rais wa Chuo cha St Joseph mjini Morogoro, Hajrath Mshamo (22), aliyekuwa akisoma mwaka wa tatu. Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Alex Mkama, alisema kwa kushirikiana na wananchi, wamekamata watuhumiwa watatu wakazi wa Morogoro.

Aliwataja waliokamatwa kuwa ni Tyson Eliakim (20), Elias Lenjement (29) na Fredrick Nogwa (21) anayedaiwa kuwakodishia pikipiki watuhumiwa wenzake yenye namba za usajili MC.285 EDX.

Kamanda Mkama alisema vijana hao walipora simu ya mwanafunzi huyo kwa lengo la kujipatia kipato na katika harakati za kupambana kuokoa simu yake mmoja wao alimchoma kisu katika maeneo tofauti ya mwili wake na kusababisha kifo chake.

Kamanda aliwataka wazazi na walezi kusimamia malezi pamoja na maadili ili vijana wajipatie kipato kwa njia ya halali na kupunguza uhalifu wa aina hiyo.

Tukio hilo lilitokea Aprili 16, mwaka huu, majira ya saa 2:30 usiku, wakati Hajrath na wenzake wakiwa kwenye hosteli za chuo hicho katika maeneo ya Mkundi, baada ya wanafunzi kumkamata kijana aliyekuwa amepakizwa kwenye pikipiki na mwenzake kukwapua simu ya mwanafunzi huyo.

# Waathirika mafuriko Lindi waomba maeneo mbadala

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAATHIRIKA wa mafuriko Mitaa ya Mtange, Kata za Jamhuri na Rupiani Manispaa ya Lindi, wameiomba serikali kuwapatia maeneo mbadala ya kuishi ili kunusuru maisha yao.

Wananchi hao walitoa ombi hilo kwa wenyeviti wa mitaa yao, Amiri Rajabu na Hatibu Mohamedi walipokuwa wanapokea msaada wa vyakula vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni nne kutoka Kamati ya Maafa ya Manispaa ya Lindi.

Msaada huo ni pamoja na unga wa mahindi, maharage, mafuta ya kupikia, sabuni na chumvi. Wenyeviti wa mitaa hiyo wamesema kutokana na maafa waliyapata mwaka huu, wapo tayari kubadilisha makazi kutoka maeneo ya mabondeni ambayo sio rafiki kwa salama wa maisha yao na kwenda kuhamia maeneo yenye miinuko.

"Tunachokuomba mkurugenzi tumia wataalamu wako idara ya aridhi kutupimia viwanja vya bei nafuu maeneo yaliyoinuka tumechoshwa na mateso haya," walisema Rajabu na Hatibu.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Juma Mnwele, ambaye pia ni Mwenyekiti wa kamati ya maafa akipokea ombi hilo, alihaidi kulifanyia kazi, huku akiwataka wanaoishi mabondeni kuchukua tahadhari ya kuishi kwenye maeneo yenye miinuko.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wananchi wake, huku akiwasisitiza kuchukua taadhari ya kuwalinda watoto, wazee wasiojiweza na wenye ualemavu kuwaangalia mara kwa mara mvua zinazopeleka maji ndani ya nyumba zao.

HABARI KITAIFA

# Samia amlilia Gardner

Na Elizabeth Zaya



RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wafanyakazi wa Clouds Media Group, kutokana na kifo cha mtangazaji wa Kituo cha Radio cha Clouds, Gardner Habash (51), aliyefariki jana.

Katika ukurasa wa X, Rais Samia aliandika; "Mchango wa Gardner kwenye ustawi wa sekta ya habari nchini ni mkubwa, na amekuwa mnasihi wa vijana wengi. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema. Amen."

Mwili Gardner unatarajiwa kuagwa leo jijini Dar es Salaam na baadaye kusafirishwa kwenda mkoani Kilimanjaro kwa maziko.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na uongozi wa Clouds Media Group, maziko yanatarajiwa kufanyika kijijini kwao Kikelelwa, Kata ya Tarakea, wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro kesho.

Ratiba hiyo ilionyesha kuwa, mwili wa Gardner ulipelekwa jana jioni nyumbani kwake Kijitonyama ambako kulifanyika ibada ya faraja kwa familia.

Kadhalika, leo saa mbili asubuhi, mwili utapelekwa kwenye viwanja vya Leaders Club vilivyopo Kinondoni, Dar es Salaam kwa ajili ya umma kupata nafasi ya kuaga.

Gardner alifariki juzi Aprili 20, mwaka huu alfajiri katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dar es Salaam alipokuwa akipatiwa matibabu.

Gardner ambaye ni baba mzazi wa msanii wa Bongofleva, Malkia Karen, anakuwa ni Mtangazaji wa pili kufariki dunia akiwa anakitumikia kipindi hicho cha Jahazi cha Clouds FM, baada ya Ephraim Kibonde, aliyefariki dunia Aprili mwaka 2021, wakati anatibiwa katika Hospitali ya Bugando, jijini Mwanza.

Sehemu nyingine ambako Gardner aliwahi kufanya kazi ni Times FM, kupitia kipindi cha Masikani, pamoja na EFM ambako alianzisha kipindi cha Ubaoni kabla ya kurejesa tena Clouds FM, mwaka 2016.

# WB yatakiwa kutoa kipaumbele Afrika

Na Scola Malinga, WASHINGTON

TANZANIA imeishauri Benki ya Dunia (WB) kuweka mbele vipaumbele vya maendeleo vya nchi za Afrika, ikiwamo kuzipatia fedha na ujuzi ili ziweze kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Rai hiyo imetolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kwenye Mkutano wa Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika la Benki ya Dunia) (WBG Africa Group 1 Constituency) uliofanyika Washington DC, nchini Marekani.

Alisema WB imekuwa inasaidia kwa kiasi kikubwa nchi za Afrika na sasa wasaidie kuwekeza nguvu zaidi kwenye miradi ya maendeleo ili kuinua uchumi kwa haraka.

"Tunaiomba WB inapopitia matarajio yao iweke kipaumbele kwa Afrika na kwa nchi moja moja na kutoa nyongeza ya rasilimali fedha," alisema Dk. Mwamba.

Aidha, aliiomba benki hiyo kupeleka fedha zitakazoongezwa kupitia mzunguko mpya wa mfuko wa IDA 21 zipelekwe moja kwa moja kwa walengwa ili kupata matokeo chanya kwa haraka

Aidha, alitoa wito kwa mashirika ya fedha ya kimataifa kutoa mikopo ya muda mrefu (Long Term Loans) isiyo na riba, ili nchi za Afrika ziweze kutekeleza miradi ya maendeleo kikamilifu.

"Mikopo ya muda mfupi inaumiza nchi za Afrika, hivyo tunaomba mikopo iwe ya muda mrefu, miaka 50 hadi 70 na isiyo na riba," alisisitiza Dk. Mwamba.

Aidha, alikumbusha ombi la Serikali ya Tanzania katika mkutano wa 26 wa kundi la kwanza la nchi za Afrika uliofanyika Marrakech, Morocco mwaka jana, la kukifanya kiswahili kuwa miongoni wa lugha za mawasiliano wakati wa mikutano yake kutokana na kukua kwa lugha hiyo na kutumika kwenye mikutano mingine mingi ya Kikanda na Kimataifa.

"Kiswahili kimekuwa moja ya lugha inayotumika katika mikutano ya Afrika Mashariki (EAC), SADC, AU na sasa inakwenda kupitishwa kutumika kwenye mikutano ya kimataifa," alisema Dk. Mwamba.

Mkutano huo ulihudhuriwa na nchi 22 wanachama ikiwa ni pamoja na Tanzania, Botswana, Burundi, Eritrea, Eswatini, Ethiopia, Gambia, Kenya, Lesotho, Liberia, Malawi, Msumbiji, Namibia, Rwanda, Ushelisheli, Sierra Leone, Somalia, Sudan, Sudan ya Kusini,Uganda, Zambia, na Zimbabwe.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kimya cha viongozi Simba hakina afya kwa mashabiki

**WANACHAMA** na mashabiki wa Simba wanapitia katika wakati mgumu kutokana na timu yao kutofanya vizuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, hivyo kuelekea kuukosa ubingwa huo kwa msimu wa tatu mfululizo.

Lakini pia katika michuano ya kimataifa, imetinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa mbinde kabla ya kuondoshwa na Al Ahly ya Misri na kushindwa kufikia lengo lao la kufika nusu fainali ya mashindano hayo.

Kadhalika, msimu huu imefungwa na watani zao wa jadi, Yanga nyumbani na ugenini, ikianza kukubali kipigo cha mabao 5-1 Novemba 5, mwaka jana, kabla ya juzi kufungwa 2-1.

Baadhi ya mashabiki na wanachama wa klabu hiyo walianza kwa kunung'unika kuwa timu yao kila muda unavyozidi kwenda badala ya kuimarika inazidi kuporomoka, ambapo walihoji tatizo ni nini? Lakini hawakujibiwa.

Wengine wakitoa maoni yao kuhusu mwenendo mbaya wa timu yao, lakini wakaitwa wachochezi.

Kwa sasa kikosi cha Simba kinaonekana kwenda, 'Mungu nisaidie', kwani msimu huu hakijawa na kiwango ambacho Wanamsimbazi wenyewe wamekizoea na wengi wanaamini kuwa usajili mbovu usiokuwa na malengo unaofanywa na baadhi ya viongozi ndiyo ulioifikisha timu yao hapo ilipo.

Hilo linadhihirishwa pia na matokeo ya hivi karibuni ya timu hiyo ambapo imetolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikichapwa bao 1-0 nyumbani na mabao 2-0, ugenini dhidi ya Al Ahly, hiyo ikiwa ni mara ya kwanza kwa timu hiyo kupata matokeo dhidi ya Simba hapa nchini.

Kama vile haitoshi, ikatolewa kwenye hatua ya 16-bora ya Kombe la FA kwa mikwaju penalti 6-5 dhidi ya Mashujaa FC, na hata iliporejea kwenye mechi za Ligi Kuu, ikakwaa kigingi cha sare ya bao 1-1 dhidi ya Ihefu FC.

Mpaka hapo tu, inaonyesha namna mashabiki wa Simba hali yao ilivyo, na wamekuwa wakilalamika, lakini hakuna kiongozi hata mmoja wa klabu hiyo aliyejitokeza na kuwaambia hali halisi ilivyo.

Mtu pekee ambaye anaonekana ni kiunganishi cha klabu, wanachama na mashabiki ni, Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, ambaye naye baada ya kipigo cha juzi, hajaongea chochote.

Viongozi wao waliowachagua na walioteuliwa wapo kimya, kama vile hakuna kinachotokea. Hali hii si nzuri hasa ikizingatiwa kuwa viongozi hao wako hapo kwa ajili ya hao hao wanachama na mashabiki.

Klabu ni kama kampuni, ama tasisi na wanachama na mashabiki ni kama wateja wa bidhaa zinazozaliswa, hawa ndiyo wanaokata tiketi kuingia viwanjani, kununua skafu, jezi na vitu vingine, hivyo kuwaacha bila kuwaambia kitu chochote ni kutowatendea haki.

Ni wajibu wa baba, mama au mzazi kuongea chochote kile pale familia inapopitia kwenye hali ngumu, ili kuwapa faraja, na matumaini hata kama hayapo. Mlezi ndiye ana dhima ya kumbembeleza mtoto anapokabiliana na hali ngumu na ya kukatisha tamaa, hivyo viongozi wa Simba hawana budi kufanya hivyo.

Tunaamini kukaa kimya namna hiyo hakuleti afya kwa maendeleo ya klabu yao, kwani viongozi hao hawataeleweka kama wakijitokeza wakati mwingine wowote, kwa kuwa kiongozi mzuri ni yule anayeongoza na kuwa na watu wake wakati wa raha na shida.

Simba ni taasisi kubwa kwa sasa kutokana na kuwa na wafuasi wengi, hilo viongozi wanapaswa kulitambua, bila hawa wanaolia na kulalamika kwa sasa hata wao wasingejivunia kuongoza klabu hiyo.

Wanachama na mashabiki wa Simba wanapaswa kuelezwe kila kitu kuhusu mwenendo wa klabu yao, ili kuilinda 'brand' klabu kimya hiki cha viongozi kinaweza kuishusha zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Viongozi wa Simba, Yanga SC wanapoteza mvuto wa 'Dabi'

**ILIKUWA** ni moja ya 'Dabi' chache zilizopooza na kutokuwa na mvuto kuanzia nje mpaka ndani ya uwanjani. Ilikuwa mechi ya kawaida sana uwanjani. Hatukuona ubunifu ambao baadhi ya wachezaji huwa wanajipambanua katika mechi za dabi.

Huko nyuma kuna baadhi ya wachezaji ambao wanakuwa hawana majina makubwa, lakini wanakuja kuyapata katika mechi moja tu ya dabi.

Sitaki kwenda miaka ya mbali sana kwa kina Said Swedi 'Scud' ambaye alipata jina kwa kuitungua Simba kutoka kuwa mchezaji wa kawaida, wala kina Ulimboka Mwakingwe, Joseph Kaniki, Dua Said ambao ustaa wao walianza pale walipoanza kuitungua Simba, kwani miaka ya karibuni tu kuna mchezaji anaitwa Shiza Kichuya, ambaye 'ujiko' aliupata katika hizi dabi kiasi cha kila shabiki wa soka mitaani hata watoto wakawa wanamfahamu.

Zamani wachezaji walikuwa wanajiandaa kufanya kitu katika mechi ya dabi ili waimbwe mechi inapomalizika. Walicheza mara mbili zaidi ya uwezo wa kawaida, walipambana na kila mmoja kucheza kwa kiwango cha hali ya juu kiasi cha kuifanya dabi kuwa na mvuto.

Pale kati ndiyo inakuwa balaa, kama ulishawahi kuona shoo za kina Issa Athumani, Athumani China, Ramadhani Lenny, Mtemi Ramadhani, Hussein Masha, Hamisi Gaga 'Gagarino', Nico Nyagawa, ilikuwa ni hatari tupu.

Nakumbuka mechi iliyopita na zingine nyuma, ilifika wakati mashabiki wanakaa mpaka kwenye ngazi za kuingilia uwanjani. Hakuna pa kutemea mate na hata kama mtu anataka kwenda msalani, atafanya hivyo na kurejea kwenye siti yake kwa shida. Hii ni miaka ya hivi karibuni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kwenye Uwanja wa Taifa (Sasa Uhuru ndiyo usiseme, miaka ya 1970 mpaka 1980, uwanja ulijaa saa nne asubuhi, huku mashabiki wakiwa amekwenda na chupa za chai, maji ya kunywa na vyakula vyao kutoka majumbani.

Leo hii ambapo mashabiki wa soka wameongezeka mara dufu, mechi ya Simba na Yanga inakuwa na watu wachache vile ni suala ambalo haliwezi kupita hivi hivi bila kuongelewa na lisijirudie tena.

Tukianza na viongozi wa Simba, Msimu huu timu imeonekana haiwaridhishi kabisa mashabiki kiasi cha kuleta tafrani kabla hata ya mechi ya dabi, baadhi wakisusa kwenda uwanjani. Wamesusa ili kupeleka ujumbe kwa viongozi kuwa hawaridhishwi na mwenendo wa timu yao na hata wao wenyewe. Wengine wakakamatwa na Jeshi la Polisi. Hawajawahi hata kutoka mbele ya wanachama na mashabiki wao kuwaambia tatizo ni nini?

Wala si siri kuwa mashabiki wa Simba ndiyo huipamba zaidi dabi kwa sababu huingia kwa wingi zaidi, ukichanganya na matarumbeta na mavuvuzela yao na aina yao ya ushangiliaji, uwanja unapendeza. Safari hii haikuwa hivyo.

Viongozi wa timu hiyo wameifanya timu imekuwa ya kawaida sana kiasi cha Simba kutoogopwa na timu yoyote, lakini hata mashabiki wao hawaiamini tena, wanaogopa kwenda uwanjani kuepuka fedheha, na wengi wanaonekana kususa.

Upande wa Yanga nawalaumu kwa kitendo chao cha kupenda kuwapa wanachama na mashabiki wao tiketi za bure katika mechi mbalimbali, hasa zile kubwa na za kimataifa.

Huu ni ugonjwa ambao wameupandikiza, kiasi kwamba inapotokea mechi ambayo wanapaswa waingie kwa tiketi za kununua inakuwa mtihani. Hawanunui kwa sababu huwa hawajipangii bajeti hiyo, au wanasubiri hadi dakika za mwisho wakidhani bure inakuja.

Inawezekana hata mechi hii kwa sababu Yanga ilikuwa ndiyo mwenyeji, walidhani dakika za mwisho wanaweza kuambiwa bure. Ndiyo maana waliokata tiketi walikuwa wachache.

Viongozi wa Yanga wanaona kama vile wanawapenda sana mashabiki wao, lakini wanafuga ugonjwa na waswahili; wanasema mwana umleavyo ndivyo akuavyo.

Dabi hii haikuwa na mashabiki wengi kwa sababu upande mmoja wamesusa, upande mwingine wamezoea bure.

Hii yote imesababishwa na viongozi wa klabu hizi kongwe nchini. Nadhani kwa dabi hii viongozi wa pande zote mbili watakuwa wamejifunza kutokana na makosa yao.

## HABARI KITAIFA

# YDF yatoa mikopo bil. 1/- kwa vijana

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema maboresho ya Mwongozo wa Utoaji Mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF), umewezesha kutoa mkopo kwa kijana mmoja mmoja, wakiwamo wenye ulemavu.

Imesema, kwa mwaka huu wa fedha mfuko huo umetoa Sh. 1,274,471,500 kwa ajili ya miradi ya vijana 56 yenye wanufaika 392.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patribas Katambi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, Katambi, katika uzinduzi wa awamu ya pili ya mradi wa kuwalinda vijana 'Safeguard Young People Programe' (SYP), jijini Dar es Salaam.

Mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) kwa ushirikiano na Ubalozi wa Uswisi nchini na Tanzania, ambao unalenga kuleta mabadiliko chanya kwa vijana.

Alifafanua, serikali inatambua vijana wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kimaisha ikiwamo afya huku baadhi wakijiua na wakati mwingine kuua watu kutokana na misongo ya mawazo.

"Kwa mujibu wa Utafiti wa Nguvu Kazi, 2021 (ILFS, 2021), Tanzania ina nguvu kazi ya watu wapatao milioni 25.8. Kati ya nguvu kazi hiyo, vijana ni milioni 14.2 sawa na asilimia 55.6.

Kadhalika, Katambi alionya vijana, hasa athari za mmomonyoko wa maadili, akisema ni tishio kubwa kwa vijana, kuliko hata maradhi, kwamba huchochea rushwa na uwajibikaji duni.

"Vijana usiwe kikwazo kuwahudumia wengine. Vijana hatupaswi kuwa wa sura hizo tofauti na maandishi ya maneno ya vitabu vitakatifu. Vijana tuache alama, alama si majumba au mali," alisema Katambi.

Alisema asasi, wadau wa maendeleo wana mchango mkubwa katika kuwatambua, kuwaonesha njia vijana na kufanikisha ndoto zao, baada ya kupatiwa mafunzo mbalimbali, kupitia mradi huo.

"Programu hii ya "Safeguard Young People" ni muhimu sana katika kutoa msaada, elimu na fursa kwa vijana wetu ili waweze kujikwamua na changamoto wanazokabiliana nazo na kufikia mafanikio katika maisha yao," alisema Katambi. Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot, alisema mwaka huu, Uswisi na Tanzania zinaadhimisha miaka 60 ya uhusiano rasmi wa kidiplomasia na tathmini ni nia ya pamoja ili kuendelea kuimarisha mahusiano haya katika maeneo ya kijamii, kisiasa, kibiashara, ubunifu, elimu na utamaduni.

"Vijana ni tayari taifa la leo. Serikali ya Uswisi, kama mshirika wa Serikali ya Tanzania, tunatambua changamoto zilizopo kutokana na kasi ya ongezeko la watu nchini Tanzania, hasa kwa vijana.

"Changamoto hizi ni za kiafya, hasa kuhusiana na masuala ya uzazi na lishe; za kiuchumi, hasa kutokana na ukosefu wa ujuzi wa kutosha na unaohitajika na ajira; na hata za kisaikolojia na kijamii," alisema Balozi Didier.

Alibainisha utatuzi wa changamoto hizo, kuwa ni pamoja na programu ya SYP, ambayo inatekelezwa zaidi ya nchi 10 Afrika; Zambia, Eswatini, Malawi, Zimbabwe, Afrika ya Kusini, Namibia, Botswana, Lesotho, Rwanda, Angola, Tanzania na Msumbiji.

Mark Bryan Schreiner, Mwakilishi wa UNFPA nchini, alisema awamu ya kwanza ya mradi huo, umefanikiwa kutokana na Serikali ya Tanzania kuwa usimamizi thabiti.

Alisema vijana wafanyie kazi ujumbe wa mradi huo ambao ni 'Kijana Changamkia Fursa; Kijana Acha Alama' ili kujiinua na kutokubali kuangushwa.

"Kwa pamoja kwa kushirikiana na vijana tunaweza kupona, kuibadili dunia na kusababisha mazuri kwa vizazi vijavyo," alisema Schreiner.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Kituo cha Afya Shehiya ya Kinyikani, Jimbo la Kojan, Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini, Pemba. Wa kwanza kulia (mbele) ni Mbunge wa Jimbo la Kojani ambaye pia ni Naibu Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hamad Chande. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko awaasa Watanzania kutokubali kugawanywa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amewaasa Watanzania wasikubali kugawanywa na badala yake waulinde na kudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao unatimiza miaka 60 Aprili 26, maadhimisho yatakafanyika jijini Dar es Salaam.

Dk. Biteko alisema kuimarika kwa Muungano kumetokana na amani, utulivu na mshikamano miongoni mwa Watanzania na ni moja ya Tunu za Taifa ambao unahitaji kulindwa ili kuenzi matunda yaliyopatikana.

Dk. Biteko aliyasema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Kituo cha Afya Shehiya ya Kinyikani Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho kuelekea miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

"Tanzania ndio nchi pekee barani Afrika na duniani kwa ujumla kuwa na Muungano imara na thabiti kwa miaka mingi, hivyo ni vema kuulinda kwa namna yoyote ile," alisema Dk. Biteko

Awali, alikagua ujenzi wa kituo hicho kinachojengwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) kwa kusimamiwa na Wakala wa Ujenzi Zanzibar (ZBA), ambao hadi kukamilika itagharimu Sh. milioni 500.

Pia amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuhakikisha miradi ya maendeleo zikiwamo zahanati, vituo vya afya, shule na miundombinu mbalimbali inatekelezwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, amepongeza jitihada zinazofanywa na Rais wa Zanzibar kwa kuwaletea wananchi maendeleo na kuhakikisha huduma za Afya zinaimarika kisiwani Pemba.

Naibu Waziri wa Fedha ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kojani, Hamad Chande, aliwashukuru wananchi wa Jimbo la Kojani kwa kuchangia asilimia 10 ya ujenzi wa kituo hicho cha afya pamoja na nguvu kazi kwenye ujenzi wa kituo hicho na kuwaahidi pindi ujenzi utakapokamilika atatoa gari la jipya la wagonjwa ili kurahisha huduma kwa wakazi wa maeneo hayo.

Kituo hicho cha afya kitakuwa na huduma mbalimbali ikiwamo ya wagonjwa wa nje (OPD), uzazi, mama na mtoto, maabara, ultra sound na huduma nyingine za tiba.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, pamoja na viongozi wengine na wawakilishi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUSSA ALLY SANGALI**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 523 DGT aina ya TATA – LP – 909 yenye Chassis namba MAT382042F7R18183. Engine namba 497TC93KUY833828. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/49672/2024.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA KINONDONI
MWANANYAMALA
SHAURI LA MADAI NAMBARI 271 LA 2023
AMINA MOHAMED
MSHINDO.........................MUOMBAJI/WAOMBAJI
DHIDI YA**

- **HUSSEN SALUM MOHAMED**
- **ABASI SAID CHINGA............MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

- **HUSSEN SALUM MOHAMED**
- **ABASI SAID CHINGA**

**POPOTE ULIPO/MLIPO:**

**AMINA MOHAMED MSHINDO** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni(mwanyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 10/06/2024 saa 03:00 Asubuhi mbele ya **Mh J.W. SILLAS** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 03 mwezi 04, 2024

MWENYEKITI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA
Kituo cha KATORO Mkoa GEITA
Shauri a madai/Ndoa Na 18/2024
Jina la Mdai: CATHERINE ERNEST
Jina la Mdaiwa: LUBANGO KISHIBA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuniya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:LUBANGO KISHIBA WA MJI MWEMA**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake YA TALAKA NA KUGAWANA MALI YA PAMOJA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 22 Mwezi 04 Mwaka 2024 saa 2.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. ANGALIZO:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 26 Mwezi 03 Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KATORO GEITA

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**HAPPY REGINALD GRATIANA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba **MC 376 ATG.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/66695/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE
Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM
Shauri la Madai/Ndoa Na. 579/2024
Jina la Mdai: MIQDAAD MOHAMEDALI RAMANI
Jina la Mdaiwa: SAYYADA NASIR TETHA
KUITWA SHAURINI
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)
Kwa: SAYYADA NASIR THETHA
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba**

**KUHUDHURIA MAHAKAMANI**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 Mwezi 04 Mwaka 2024 saa 3:30 asubuhi mbele ya Mhe. MLAPONI Hakimu Mkazi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinvyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama leo tarehe 18 Mwezi 04 mwaka 2024.

HAKIMU

# NEMC yaonya wanaojenga bila tathmini mazingira

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewaonya watu wanaojenga miradi bila kupata Cheti cha Tathmini ya Mazingira (EIA) kwamba wanakabiliwa na faini ya Sh. milioni 10.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam na msosholojia wa Baraza hilo, Suzan Chawe, wakati akizungumza kwenye ufunguzi wa maonyesho ya kumbukumbu ya miaka 60 ya Muungano.

Suzan alisema NEMC inafanya ukaguzi wa mara kwa mara na wanaokutwa wamejenga miradi bila EIA hutozwa faidi hadi Sh. milioni 10.

Alisema NEMC inaendesha kampeni ya elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa EIA kwa wanaojenga miradi kabla ya kufanya ukaguzi na kuwatoza faini.

"Mfano unaweza kukuta mtu anajenga kituo cha mafuta kwenye makazi ya watu jambo ambalo ni hatari kama ikitokea dharura tunaweza kupoteza maisha ya watu kwa hiyo tunasisitiza umuhimu wa EIA kabla ya kuanza shughuli za ujenzi," alisema Suzan. Alisema kwa miaka 60 ya Muungano, NEMC inajivunia mambo mengi ikiwamo kupigania ustawi wa mazingira kwa kuhakikisha miti mingi inapandwa na kulindwa.

Suzan alisema Baraza limefanya maboresho ya mifumo yake ya mapito ya taarifa za tathmini na kaguzi za athari kwa mazingira kwa kuimarisha miundombinu ya TEHAMA kulingana na matakwa ya mfumo wa serikali mtandao.

Alisema NEMC inasimamia miradi inayofanya tathmini ya athari kwa mazingira kwa njia ya kielektroniki kupitia usajili wa mtandaoni.

Alisema njia hiyo inamuwezesha mwekezaji kuanzisha mchakato wa kupata cheti cha EIA kupitia mfumo wa usimamizi wa mradi (Project Management System). "Kabla ya kufanya usajili wa mradi mwekezaji anatakiwa kuhakikisha mawazo ya wadau yamepatikana kuhusu utekelezaji wa mradi kwenye eneo husika," alisema Suzan.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Kinondoni, Stellah Walingozi (wa pili kushoto), akikabidhi kadi ya uanachama wa Umoja wa Wazazi Tanzania kwa mmoja wa wanachama wapya, wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Umoja wa Wazazi Kata ya Wazo, yaliyofanyika katika ofisi ya CCM Tawi la Wazo, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Katibu wa Wazazi wa Kata hiyo, Rehema Salama. **PICHA: JOHN BADI**

# Wafurahia mradi kuwapatia majisafi na salama

**Na Steven William,** MUHEZA

WANANCHI wa Kijiji cha Magodi, Kata ya Parungu Kasera, Wilaya ya Mkinga, wamemshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia majisafi na salama kupitia ujenzi wa mradi wa kisima cha maji chini ya ufadhili wa taasisi ya Islamic Help.

Kisima hicho chenye thamani ya Sh. milioni 15, kilianza kujengwa tangu Machi 8, mwaka huu na kukamilika Aprili 10 kwenye eneo la Zahanati ya Magodi ambacho kitatoa huduma ya majisafi kwa wagonjwa na wakazi wa eneo hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga, Dk. Salvio Wikesi, ambaye pia ni Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, aliishukuru taasisi hiyo na Rais Dk. Samia kwa kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kuungana na serikali kutatua kero za wananchi.

"Januari 25, mwaka huu tulipata ugeni wa Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko kuzindua mradi wa REA katika Zahanati ya Magodi, alipowauliza changamoto wananchi, mkasema paa la zahanati linavuja pamoja na shida ya maji, akatoa fedha zake mfukoni kukarabati paa la zahanati hiyo na akamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha kisima cha maji kinachimbwa ili kusaidia upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi, leo tunashuhudia Taasisi ya Islamic help imetukabidhi mradi huu tunawashukuru sana," alisema Dk. Wikesi.

Naye Mratibu wa Idara ya Maji kutoka Taasisi hiyo, Nasibu Sheguni, alisema wanaishukuru serikali kuanzia ngazi ya msingi hadi wilaya kwa sapoti kubwa waliowapa mpaka kukamilisha mradi huo wa kuchangia jitihada katika kuziendelea jamii kupitia huduma ya majisafi na salama.

Pia, Mwenyekiti wa kijiji hicho, Jackson Banda alimshukuru Rais Dk. Samia kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wafadhili hao kusaidia wananchi ikiwamo upatikanaji wa majisafi na salama kijijini hapo.

# Walioathiriwa mafuriko Kibiti wasaidiwa chakula, vifaa

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

KUTOKANA na mafuriko yaliyotokea katika Halmashauri ya Kibiti na kusababisha athari kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa Mto Rufiji, wadau mbalimbali wanaendelea kujitokeza kutoa misaada ikiwamo ya chakula kuwawezesha kuishi kupata huduma muhimu kama awali.

Mkuu wa wilaya hiyo, Kanal Joseph Kolombo, amekuwa akitoa taarifa ya kuomba wadau mbalimbali kujitokeza kusaidia walengwa ambao nyumba zao zimezingirwa na maji huku mazao yao yakiharibika.

Juzi Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi Tanzania (UWT), ulikuwa ni kati ya waliojitokeza kutoa misaada kwa waathirika wa mafuriko.

Akikabidhi misaada hiyo, Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda, alisema katika kipindi hiki wakazi wa maeneo ya delta katika wilaya za Kibiti na Rufiji, wanatakiwa kuacha kutumia usafiri wa mitumbwi kuepusha hatari ya maisha yao kutokana na wingi na kasi ya maji yanayopita katika Mto Rufiji.

Chatanda alimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, vifaa mbalimbali vilivyotolewa na Jumuiya hiyo ambavyo ni pamoja na shuka 470, vyandarua 400, vijora 500, unga wa sembe viroba 76, maharage kilo 100, sukari kilo 150, nguo mchanganyoko na ndoo ndogo na kubwa za plastiki 380.

Vifaa vingine vilivyotolewa ni mabeseni 400, sahani 442, vikombe 492, magodoro 47, nguo za watoto belo moja, nguo za watoto wa kike belo moja, nguo mchanganyiko, mabegi ya shule 35, taulo za watoto viatu na tambi, mablanketi na vitu vingine ambavyo vitawasaidia waathirika waliopo kambini.

Akishukuru baada ya kupokea msaada huo Mkuu wa Mkoa wa Pwani, aliwahakikishia itasimamiwa na kuwafikia walengwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kanali Joseph Kolombo, akipokea misaada hiyo alisema bado wanaendelea kupokea misaada na kuisafirisha kwenda kwa waathirika 2,472 walioko kambi nne za Kitumbini, Mtombori, Kibongoya na Mkwajuni.

"Niendelee kuishukuru serikali na wadau wanaoendelea kutuletea misaada ambayo hadi sasa tumepokea unga tani 76, maharage tani 17, magodoro 742, nizidi kuwaomba wadau kujitokeza na kuwaahidi misaada yote waliyotoa itapelekwa kwa walengwa kama tunavyofanya," alisema.

Wilaya ya Kibiti na Rufiji wananchi wake wanaoishi pembezoni mwa Bonde la Mto Rufiji, nyumba zao zimezingirwa na maji na kulazimika kuhama kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha huku mazao yao yakiharibiwa na mafuriko.





Meneja wa Bandari ya Tanga, Masoud Mrisha akizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari waliotembelea bandari hiyo, jijini Tanga mwishoni mwa wiki, kuona maboresho yaliyofanyika. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wanafunzi MoCU wahoji kukosekana ushindani katika ajira, fursa za uchumi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JUMUIYA ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), imetaka kutafutwa 'mwarobaini' wa tatizo la kukosekana kwa ushindani sawa kwenye fursa mbalimbali za kiuchumi, ajira na maeneo mengine.

Kutokana na kilio hicho, serikali imeelekeza asasi za kiraia zinazojihusisha na jamii ya watu wenye ulemavu, kuingia kazini kuhamasisha makundi hayo kuanzisha miradi na kuisajili, ili Ofisi ya Waziri Mkuu itakaporuhusu kuanza kutolewa kwa mikopo ya asilimia 10, baada ya majaribio katika Halmashauri 10 nchini wapewe kipaumbele.

Akizungumza jana katika siku ya watu wenye mahitaji maalum katika chuo hicho, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Talky Mohamed, alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na chuo hicho dhidi ya kundi hilo, bado yako mambo yanahitaji utatuzi wa haraka ili mazingira yao ya kujisomea yazidi kuwa bora zaidi.

"Kwa mfano MoCU tunao wanafunzi 15 wenye changamoto za usikivu lakini kifaa kilichotolewa na serikali ni kimoja tu. Vilevile tunao wanafunzi 10 wenye changamoto za viungo lakini viti mwendo tulivyopewa mwaka jana ni vitatu; na mwaka huu tukapewa babaji mbili na hatukubahatika kupata viti mwendo," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo, Kurugenzi ya Huduma za Wanafunzi MoCU, Dk. Elisifa Nnko, alimwomba Naibu Meya wa Manispaa ya Moshi, Stuart Nathaniel, kuona namna kuisemea jamii ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, kwa kuwajengea mazingira ya kupata fursa mbalimbali za kiuchumi, wakati mwingine fursa mbalimbali za kielimu.

"Ni ombi letu kama jamii ya watu wenye mahitaji maalum hilo ulichukue na pale ambapo mazingira yatakuwa yanaruhusu tafadhali usilihasau kusanyiko hilo la MoCU, kwa kuwa tunajua linamchango mkubwa katika jamii na katika taifa," alisisitiza Dk. Nnko.

Akijibu ombi hilo, Naibu Meya aliwadokeza wanafunzi hao wenye mahitaji maalum kuwa mpaka kufikia Machi mwaka huu, Halmashauri ya Manispaa hiyo, tayari ilikuwa imetenga asilimia mbili ya fedha za ruzuku kwa ajili ya mikopo ya wenye ulemavu zaidi ya Sh. milioni 260.

"Fedha hizo zilizoko katika Halmashauri yetu ya Manispaa ya Moshi, maana yake ni asilimia 20 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya asilimia mbili. Ukitafuta asilimia 20 hapo, utaona kuna Sh.milioni 260. Tutakaporuhusiwa kuanza kuzitoa naomba mjitokeze.

"Hii asilimia mbili kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum, niwaombe taasisi zote ambazo tunashirikiana nao zikiwamo asasi za kiraia pamoja na klabu tubuni shughuli mbalimbali ambazo tutaweza kuzifanya.

...Labda niwaambie tu, mpaka kufikia Machi mwaka huu, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, ilikuwa na zaidi ya Sh. bilioni 1.3 ya fedha hizo, japokuwa mfuko huo ulisimamishwa kwa muda lakini halmashauri zimekuwa zikiendelea kutenga zile fedha na kuziweka.

Katika hafla hiyo, Rais wa Serikali ya Wanafunzi chuoni hapo (MoCUSO), Yohana Kazimili, alisema mtu anaweza akakataa jinsi mtu mwenye mahitaji maalum alivyo, akakataa muonekano wa maisha yake, akakataa ngozi yake, lakini hawezi kukataa uwezo wake.

# UVCCM: Kurudishwa mikopo 10% kutainua nuru iliyopotea

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Arusha, umesema kurejeshwa kwa mikopo ya asilimia 10 kwa halmshauri mbalimbali nchini, kutainua nuru iliyoanza kupotea na kukifanya chama hicho kuangaliwa tofauti na jamii.

Mwenyekiti wa UVCCM, Mkoa wa Arusha, Simon Maximilian, alisema hayo jana, huku akiwasisitiza vijana wote wa mkoa huo, bila kujali itikadi zao za vyama vya siasa, kujitokeza kwa wingi kuomba mikopo hiyo, ili iwawezeshe kujiajiri na kukuza uchumi wao.

Alisema kitendo cha serikali kuwajengea uwezo maofisa maendeleo ya jamii kabla ya kuanza kutolewa mikopo hiyo, kutawasaidia kusimamia utoaji wa mikopo hiyo.

Alisema serikali imeongeza idadi ya wasimamizi wa mikopo ngazi ya kata, ambapo maofisa maendeleo ya jamii 787 wameajiriwa na kupangiwa kwenye kata zilizokuwa na upungufu.

Kwa mujibu wa Maximilian, utoaji wa mikopo hiyo kupitia benki utasaidia vijana wengi kuwa na nidhamu ya fedha, uwajibikaji pamoja na ubunifu katika shughuli zao za ujasiriamali na kurejesha mikopo hiyo kwa wakati.

Aidha, alitumia fursa hiyo kuwataka vijana kushirikiana na maofisa maendeleo ya jamii ngazi ya kata ili waweze kuandika maandiko yatakayofuata mfumo unaohitajika, wakidhi vigezo vya kupata mikopo.

Katika hatua nyingine Maximilian alizitaka mamlaka zote zilizopewa dhamana ya kusimamia utoaji wa mikopo hiyo, kutekeleza wajibu wao kikamilifu kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili mikopo hiyo inufaishe walengwa na siyo vinginevyo.

# Makonda ataka 'speed' ukarabati Uwanja Sheikh Amir Abeid

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda amewaagiza mafundi wanaokarabati Uwanja wa Sheikh Amir Abeid wa jijini Arusha, kuongeza bidii kwa kuwa uwanja huo utatumika katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, Mei Mosi kitaifa.

Aidha, alisema katika maadhimisho hayo Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Makonda aliyasema hayo jana alipokagua uwanja huo na kujionea hali ya maandalizi inavyoendelea akiwa ameongoza na baadhi ya wajumbe wa kamati ya maadilizi ya kitaifa iliyoongozwa na Rais wa Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Tumaini Nyamhokya.

"Maandalizi yanaendelea vizuri lakini niwaombe mafundi wanaofanya kazi ya ukarabati wa majukwaa na maeneo mengine madogo madogo waongeze juhudi ili ukarabati huu umalizike kwa wakati kwa kuwa siku zilizobakia ni chache," alisema.

Nyamhokya alimhakikishia mkuu huyo wa mkoa kuwa maandalizi yote yanaendelea vizuri na kamati zote zilizoundwa zinaendelea na majukumu kikamilifu ili maandalizi yakamilike ndani ya muda ulipangwa.

Alisema: "Hapa kuna kamati mbalimbali ambapo kila kamati imepangiwa majukumu yake na wanaendelea nayo, lengo likiwa ni kuhakikisha maadhimisho haya yanafana na kufanyika kama ilivyopangwa"

Kwa mujibu wa Nyamhokya maadhimisho hayo yanafanyika jijini Arusha na ni fursa ya kipekee kwa wananchi wa mkoa huo, kufanya biashara kutokana na idadi kubwa ya wageni mbalimbali watakaofika katika maadhimisho hayo.

Alisema: "Ujio wa maadhimisho haya katika mkoa huu wa Arusha kufanyika jijini hapa ni fursa ya kipekee ya wanachi mkuu huu kuchangamkia fursa za biashara ili kujipatia kipato.

"mpaka sasa wameshawasili watu zaidi ya 2,000 wakiwemo wachezaji wanaoshiriki mashindano mbalimbali, kuelekea katika maadhimisho haya na hoteli nyingi kwa sasa zimejaa kutokana na mkoa huu kuwa kitovu cha utalii hapa nchini".

Alisema Siku ya Wafanyakazi Duniani hufanyika kila Mei Mosi ikiwa ni siku ya mshikamano kwa wafanyakazi wa sekta zote katika kusimamia na kuunga mkono haki, wajibu na dhamana ya wafanyakazi kote ulimwenguni katika mchakato wa kufikia maendeleo endelevu.





Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (katikati) akikabidhi cheti cha kuhitimu kidato cha sita kwa mwanafunzi wa Shule za Sekondari Kaizirege na Kemobos, Nice Kailembo katika mahafali ya shule hizo, mjini Bukoba, mkoani Kagera juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa shule hizo, Eusto Kaizirege. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zahanati yashindwa kukamilika miaka 12, wajawazito wajifungulia nyumbani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kijiji cha Tulole Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga hawana kituo cha afya, hali inayowalazimu wajawazito kujifungulia nyumbani.

Hivyo, wameiomba serikali kukamilisha ujenzi wa zahanati waliyoijenga tangu mwaka 2012 ili kunusuru maisha yao kunakohatarishwa na kukosa huduma za afya.

Waliyasema hayo wakati wa kikao na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alipofanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi.

Wananchi hao walisema ili kupata huduma ya afya wanalazimika kutumia usafiri wa pikipiki na baiskeli mpaka Kituo cha Afya Iyenze na Kilango.

Mkazi wa Kitongoji cha Ntungulu, Aziza Kitundu alisema, ukosefu wa zahanati unasababisha wajawazito wengi kujifungulia njiani wakielekea kituo cha afya kupata huduma.

Alisema wengine wanajifungulia nyumbani na kuzalishwa na watu wasiokuwa na ujuzi wowote, hali inayowatia shaka ya kuhatarisha usalama wao.

"Mwaka 2004 nilijifungulia njiani wakati naelekea hospitalini nilizalishwa mtoto wangu na mama mmoja aliyefahamika kwa Elizabeth Andrea na alikuwa anapita tu, asingekuwa huyo naimani ningepoteza maisha. Mungu ni mwema mpaka mtoto wangu yuko hai na anaendelea na masomo yake," alisema.

Kasana Lushinge alisema ili kufika Kituo cha Afya cha Iyenze na Kilango kwa pikipiki nyakati za mchana gharama ni Sh.5,000 na usiku ni Sh.15,000 hadi 20,000.

Diwani wa Kata ya Kilago, Charles Masele alisema baada ya kuwepo kwa matukio hayo wananchi walilazimika kuchangisha fedha na kupata Sh.milioni 9.17 na kuanzisha ujenzi wa zahanati mwaka 2012.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Dk. Malunde Fredrick akitoa taarifa ya ujenzi alisema ujenzi wa zahanati hiyo ulianzishwa na wananchi kwa lengo la kuondoa adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za matibabu ikiwemo ya uzazi na upasuaji.

Alisema, mpaka sasa zimeshatumika Sh.milioni 69.9 kati ya hizo Sh.milioni 48 ni fedha kutoka serikali kuu, Sh.milioni 25.6 ni mapato ya ndani ya halmashauri, huku Sh.milioni 9.173 ni fedha kutoka kwa wananchi na sasa ujenzi umefikia asilimia 98.

Alisema kwa sasa kilichobaki ni vyoo na kichomea taka na kabla ya mwaka huu kuisha kitakuwa kimekamilika.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita alisema serikali imekuwa mstari wa mbele kusogeza huduma karibu na wananchi na kuhakikisha ikamilisha miradi yote iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Alisema fedha za mapato ya ndani ya halmashauri na zile za serikali kuu zinatoka kwa awamu hasa pale zinapopatikana na ndio sababu ya zahanati kuchukua muda mrefu kukamilika.

# Bosi NMB ataka vijana wapewe elimu ya fedha, bajeti mapema

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

OFISA Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna ametoa ushauri kwa wazazi na walezi nchini kuwafundisha mapema watoto wao masuala ya fedha na upangaji bajeti ili kuwawezesha kuishi kutokana na uhalisia wa vipato vyao.

Alitoa ushauri huo katika hotuba yake wakati wa mahafali ya kidato cha sita katika Shule za Sekondari za Kaizirege na Kemebos, mjini Bukoba, mkoani Kagera mwishoni mwa wiki.

Alisema watoto wakipata elimu ya masuala ya fedha mapema, watakuwa waadilifu, watapanga maisha yao kwa kuzingatia bajeti inayotokana na vipato vyao hata baadaye kuwekeza kwa uadilifu kwenye miradi ya kiuchumi.

"Tuanze kuwajengea vijana wetu uelewa wa masuala ya fedha wakati huu ambao bado ni mapema, wakipata elimu ya masuala ya fedha wataweza kupangalia vyema maisha," alisema Zaipuna. Pia alisema kuwa ili kulisaidia kundi hilo, benki ya NMB ilianzisha jukwaa maalum la vijana liitwalo "Go na NMB" ambapo wanafundishwa masuala ya fedha na jinsi ya kujiwekea akiba na kutumia huduma mbalimbali za kidijitali zinazotolewa na benki hiyo. Zaipuna katika hafla hiyo alitoa wito kwa vijana kujiunga na jukwaa hilo kwa ajili ya kupaa maarifa ya masuala ya kifedha ambayo yatawasaidia katika safari ya maisha yao huku akiwakumbusha kuwa kutokana na mabadiliko mbalimbali hasa ya kiteknolojia, wanatakiwa kujifunza mambo mengi, kuwa wadadisi na wabunifu.

Alisema benki ya NMB imeendelea kuunga mkono ukuaji wa sekta ya elimu nchini, ikiwa ni pamoja na kutoa ufadhili wa masomo na vifaa kwa wanafunzi wanaojiunga vyuo vikuu wanaotoka kwenye familia zenye uwezo mdogo ambao wamefaulu vizuri. Alisema zaidi ya wanafunzi 130 wanaendelea kunufaika na ufadhili huo.

Katika risala yao kwa niaba ya wahitimu wa shule zote mbili za Kaizirege na Kemebos, wanafunzi Zubeda Kinono na Avin Mutegeki walisema matumaini yao ni kufanya vizuri katika mitihani yao na kujiunga vyuo vikuu.

Walisema kama walivyovumilia changamoto katika safari yao, pia watahakikisha wanaonesha juhudi katika masomo yao kwenye taasisi za elimu ya juu ili baadaye walitumikie Taifa kwa uadilifu kupitia sekta mbalimbali.

# FCT yasikiliza, kutoa maamuzi mashauri 429 kwa miaka 17

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

KAIMU Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Daniel Machunda amewaomba wadau kuendeleza ushirikiano na Baraza la Ushindani (FCT) katika kuongeza uzoefu, ufanisi katika majukumu mbalimbali.

Aliyasema hayo juzi wakati akifunga semina ya wadau wa FCT mkoani hapa, kusema kuwa semina hiyo ni muhimu kwani elimu waliyoipata itawasaidia kutambua haki na kujua wajibu wao.

"Natoa shukurani kwa baraza hili na Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya semina mkoani hapa na kuwapatia elimu wadau hawa ambao wamepata fursa ya kutoa ushauri wa kuboresha mawasiliano na baraza katika masuala mbalimbali na leo ni sehemu ya wao kutatua matatizo mbalimbali ya ushindani wa biashara na udhibiti wa soko,"alisema Machunda.

Kaimu Msajili na Mkuu wa FCT, Kunda Mkenda alisema wamesajili mashauri 442, kati ya hayo 429 yamesikilizwa na kutolewa maamuzi na baraza hilo katika kipindi cha mwaka 2007 hadi Machi mwaka huu. Alisema FCT limefanikiwa kushughulikia mashauri yalioletwa mbele yake kwa asilimia 97.1, huku mashauri 13 yaliobaki yapo kwenye hatua mbalimbali za usikilizwaji.

Alisema kutokana na matatizo yanayojitokeza na watu wengi kutolijua baraza hilo kwa mara ya kwanza wameamua kufanya semina hiyo kwa wadau mbalimbali mkoani hapa ili waweze kujua haki zao, umuhimu wa baraza na kazi zake.

Mwenyekiti wa umoja wa wajasiriamali wabunifu Tanzania, Fabiani Semba alisema kupitia semina hiyo ameweza kufahamu sehemu ya kwenda

Alisema katika sekta ya mawasiliano kumekuwa na mambo mengi yakitokea, huku wakiwa hawajui sehemu ya kwenda kutoa malalamiko pindi wanapapata matatizo.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo(TCCIA), Mkoa wa Mwanza, Gabriel Kenene, alisema amejifunza namna ambavyo rufaa zinavyopatikana na kutolewa.

Hivyo, alitoa wito kwa wafanyabiashara wanapoona hawajatendewa haki na mamlaka kama LATRA ni vizuri wakafuate haki yao kupitia baraza hilo kwani gharama zao ni ndogo.

NIPASHE JUMATATU APRILI 22, 2023
Nipashe
Spotika



JE WAJUA HARRY KANE.... UK. 14



Alexis Mac Allister

## ISIKUPITE

LICHA ya mshambuliaji wa Arsenal Leandro Trossard, kucheza mechi nyingi akitokea benchi kuliko alizoanza kwenye Ligi ya England kwa 'The Gunners', amekuwa akifunga mabao muhimu. Tangu mwanzoni mwa mwezi uliopita pekee, amefunga bao la ushindi dhidi ya Porto kwenye Ligi ya Mabingwa, bao la kusawazisha katika mechi ya robo fainali nyumbani dhidi ya Bayern Munich, na sasa juhudi zake za hivi punde - ambazo zinamfanya kufikisha mabao 14 kwa msimu huu kwenye mashindano yote. Bukayo Saka pekee ndiye aliyefunga zaidi yake kwa Arsenal.



# MASHUJAA 6 WASIOIMBWA KWENYE LIGI KUU ENGLAND

**LONDON,** England

MSIMU wa Ligi Kuu England, maarufu kama EPL, unapokaribia kumalizika, wachezaji wengi nyota wanatarajiwa kujitokeza katika michezo mikubwa zaidi ili kubaini taji litaishia wapi.

Kuanzia Kevin De Bruyne, Bukayo Saka hadi Mohamed Salah, timu sita za juu zina wachezaji wengi nyota ambao wanaweza kujitoa wakati huu, lakini zaidi ya klabu pia zinategemea mashujaa wengine kubeba mizigo pia.

Hapa tunawaangalia wachezaji sita mashujaa ambao hawaimbwi kwenye Ligi Kuu England twende sasa...

**Arsenal - Gabriel Magalhaes**

Ingawa patina wake wa kati William Saliba anaweza kusifiwa zaidi, Gabriel ana msimu mzuri wa kimya kimya kwa Arsenal.

Akiwa ameshinda vita 72 vya anga na kuokoa hatari 77, bila shaka Mbrazil huyo ndiye beki hodari na anayeona hatari zaidi kwa kikosi cha Mikel Arteta.

Gabriel aliwasili Emirates mwaka 2020 akiwa na umri wa miaka 22, kutoka Lille ya Ufaransa. Amefunga mabao manne msimu huu akiwa na 'Washikabunduki' hao, na bao lake la hivi karibuni ni katika ushindi la 6-0 dhidi ya West Ham, Februari.

**Liverpool - Alexis Mac Allister**

Msimu huu umezingatia sana mchango wa wachezaji kama Mohamed Salah, Darwin Nunez na Virgil van Dijk katika harakati za Liverpool kuwania taji.

Lakini pia kelele nyingi zinapaswa kupigwa juu ya Alexis Mac Allister, akiwa amechangia kwa kiasi kikubwa katikati ya safu ya kati ya 'Wekundu' hao tangu ajiunge na klabu hiyo kwa ada ya pauni milioni 35.

Jurgen Klopp alifanya jukumu lake kumleta raia huyo wa Argentina pale Anfield msimu uliopita wa msjirs ys joto na amethibitisha thamani yake iwe ni katika kikosi cha kwanza au akitokea benchi. Katika mechi zake saba zilizopita za Ligi Kuu England, Mac Allister ameibuka na mabao matatu na asisti nne.

**Man City - Stefan Ortega**

Ni vigumu kumtaja mtu yeyote katika timu ya Manchester City kama 'shujaa asiyejulikana,' lakini ikiwa kuna jina moja linalostahili kutambuliwa zaidi basi ni Stefan Ortega.

Ortega aliwasili Etihad majira ya joto yaliyopita huku Zack Steffen akiondoka kwa mkopo, na Mjerumani huyo amejidhihirisha kuwa msaidizi bora zaidi wa Ederson. Kwa hakika, baadhi ya mashabiki wa City bado wanahoji kwamba Ortega hutoa thamani zaidi kuliko Ederson kama kipa chaguo la kwanza.

Hakika aliwavutia mashabiki Jumamosi iliyopita, akimkwepa mshambuliaji wa Crystal Palace, Jean-Philippe Mateta na kuiwahi pasi kutoka kwa Rodri.

**Aston Villa - Matty Cash**

Kuna utata labda ikizingatiwa kwamba yeye si jina la mara kwa mara katika kikosi cha kwanza na kwa sasa hana jeraha, lakini mchezaji huyo wa Kimataifa wa Poland, Matty Cash ni mlinzi anayetamaniwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England.

Mbio zake bila kuchoka na uchezaji wake wa kushambulia umekuwa muhimu kwa mafanikio ya Aston Villa msimu huu, huku vijana wa kocha Unai Emery wakiwania kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Cash alianza uchezaji wake katika Klabu ya Wycombe Wanderers na baadaye akademi ya FAB kabla ya kusaini mkataba wake wa kwanza wa soka la kulipwa pale Nottingham Forest, na kujiimarisha kama beki wa kulia wa kikosi cha kwanza. Alijiunga na Villa mnamo Septemba 2020.

**Tottenham Hotspur - Pedro Porro**

Ni klabu gani ya Ligi Kuu England ambayo haiwezi kumtaka raia huyo wa Hispania kwenye timu yake?

Pedro Porro anastawi chini ya kocha Ange Postecoglou, akiwa amecheza mechi 27 akiwa na Tottenham Hotspur na kukamilisha dakika 90 kamili katika mechi 26.

Zaidi ya hayo, beki huyo wa kulia mwenye umri wa miaka 24, ametoa pasi za mabao saba, sawa na James Maddison na Brennan Johnson - dhihirisho la kweli la jinsi alivyo bora kwa Spurs msimu huu.

**Man United - Kobbie Mainoo**

Katika msimu uliokumbwa na utendaji duni na kukatishwa tamaa kwa 'Mashetani Wekundu', Kobbie Mainoo ameibuka kuwa nyota.

Mainoo alianza mechi yake ya kwanza ya ligi kwa Manchester United msimu huu mwishoni mwa Novemba, katika ushindi wa 3-0 wa Ligi Kuu ugenini dhidi ya Everton, na kujishindia tuzo ya mchezaji bora wa mechi hiyo.

Hivi karibuni kinda huyo alimzidi akili kiungo wa kati, Enzo Fernandez wa Chelsea weye thamani ya pauni milioni 106 pale Stamford Bridge na pia alifunga bao zuri dhidi ya mahasimu wao Liverpool, na kuthibitisha kwa mara nyingine ni kwa nini wengi wamemtaka aanze katika safu ya kiungo ya Timu ya Taifa ya England, maarufu kama 'Simba Watatu' kwenye Euro 2024.

# WACHEZAJI WA5 ARSENAL INAOPASWA KUWASAJILI




**LONDON,** England

BAADA ya msimu wa Ligi Kuu ya England wa 2022/23, ambao ulishuhudia Arsenal ikishindania taji, mashabiki wengi wa soka, au angalau mashabiki wa Arsenal, walitarajia 'Washikabunduki' hao kupeleka mchezo wao katika kiwango kinachofuata msimu huu, lakini mambo hayajawa hivyo hadi sasa kwa vijana hao wa Mikel Arteta.

Arsenal tayari wako nje ya Kombe la Ligi na la FA, wakifungwa na West Ham United na Liverpool, na ingawa bado wako kwenye mbio za ubingwa na Ligi ya Mabingwa Ulaya, mechi na matokeo fulani yamekuwa sababu ya wasiwasi.

Arsenal wametatizika kufunga mabao msimu huu, na kupata ugumu wa kucheza dhidi ya timu nyingine na wakati mwingine wamekuwa wakitabirika sana.

Zaidi ya hayo, majeraha, ulinzi duni, upana wa kikosi, uchovu, kufanya maamuzi mabaya, na kutokuwa hatari mbele ya lango kumeathiri sana Arsenal msimu huu.

Baadhi ya masuala haya yanaweza kutatuliwa kwenye uwanja wa mazoezi, lakini Arsenal wanahitaji usajili wa wachezaji wachache wenye ubora ikiwa watazingatiwa kuwa sawa na Manchester City.

Usajili mmoja au wawili katika dirisha la usajili la Januari kungeweza kuwasaidia kutwaa ubingwa kwa muda wote uliobakia, lakini hawakufanya hivyo, hata hivyo wanahitaji kufikiria kwa muda mrefu.

Arsenal watahitaji kutumia aina ya fedha walizotumia kwa Declan Rice na Kai Havertz kwa mara nyingine tena kama wanataka kurejea kilele cha mlima huo.

Hapa kuna wachezaji watano ambao Arsenal wanapaswa kupambana kuwapata...

**#1. Ivan Toney**

Ivan Toney amekuwa kwenye vyombo vya habari hivi karibuni kwa sababu ya kusimamishwa kwa kucheza kamari kabla ya kurejea tena, lakini mshambuliaji huyo pia anachukuliwa kuwa mchezaji moto zaidi katika soka la Uingereza.

Klabu nyingi ikiwamo Chelsea na Arsenal zimeonesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, na anajumuisha kila kitu ambacho timu inahitaji kutoka kwa mfungaji mabao. Akiwa amepitia ligi za chini nchini England, Toney sasa amethibitisha kuwa ni mfungaji mzuri kwenye ligi hiyo.

Yeye ni tishio kubwa la anga kutokana na nguvu na akili yake, na mtindo wake wa uchezaji utasaidia na kizuizi cha chini. Brentford inalijua hili na itataka pauni milioni 100.

Ikiwa ripoti zitaaminika, Toney ataondoka Brentford katika msimu wa majira ya joto, na ikiwa vita vya zabuni vitatokea, bei yake itapanda tu. Hii inaweza kuwaweka mbali Arsenal, lakini ikiwa majira ya joto yaliyopita yalikuwa ya kupita, basi inathibitisha kwamba Arsenal hawaogopi kutumia fedha nyingi kwa mchezaji mmoja.

**#2. Jorrel Hato**

Jina la Jorrel Hato limekuwa likivuma sana hivi karibuni huku Arsenal wakidaiwa kutaka kumsajili. Ingawa Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 17, anaonekana kukaribia kuongeza mkataba wake na Ajax, uvumi unaenea kwamba 'Washikabunduki' hao watakuwa na nia ya kukamilisha dili hilo msimu wa majira ya joto.

Hato amekuwa mwanga mkali katika msimu ambao umekuwa wa kukatisha tamaa kwa Ajax hadi sasa na ana uwezo wote unaohitajika kwa beki wa kisasa. Amecheza mechi 15 kwa Ajax msimu huo na ameendelea kuwa mmoja wa wachezaji wao muhimu zaidi.

Hato ni mlinzi mwenye nguvu, mwepesi, na urefu wa futi sita, anatawala sana angani. Kuongeza juu ya hilo kupita kwake, kukaba na kuzuia ni miongoni mwa uwezo wake. Anaweza kucheza kama beki wa kati wa upande wa kushoto katika mfumo wa ulinzi wa wachezaji watatu na uwezo wake mwingi utakuwa mzuri kwa Arteta, ambaye mara nyingi hubadilisha jinsi timu yake inavyojipanga.

Kwa kuzingatia sifa zake kama mchezaji, kuhamia Arsenal litakuwa jambo linalofaa. Arteta ni aina ya kocha ambaye anapendelea wachezaji wa aina mbalimbali na Hato ameonesha hilo. Kucheza na Timber msimu uliopita kunaweza kumsaidia kutulia Arsenal haraka.

**#3. Goncalo Inacio**

Goncalo Inacio ni beki mwingine ambaye alihusishwa na kuhamia Arsenal Januari, lakini uhamisho ulishindwa kutokana na ada yake ya uhamisho. Ripoti zinaonesha kuwa klabu ya Inacio iko tayari kumwacha aondoke, lakini iwapo tu klabu zitaweza kufikia kifungu chake cha pauni milioni 52.

Ni sawa na kusema kwamba mbali na William Saliba na Gabriel, orodha ya mabeki wa Arsenal haiko kwenye kiwango sawa, na ilionesha msimu uliopita kufuatia majeraha ya Saliba. Kumsajili Inacio kunaweza kuwa suluhu la tatizo hili, na uchezaji wake Sporting msimu huu hadi sasa ni dhihirisho la jinsi alivyo na anaweza kuwa bora katika siku zijazo.

Inacio atakuwa kiungo bora kwa safu ya nyuma ya Arsenal, na ushindani wa kucheza kila mchezo utafanya kila mtu kuimarika. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ndiye hasa Arteta anamtaka. Hababaiki na mpira miguuni mwake na anapenda kubeba mpira mbele, na licha ya kukosa urefu, yeye hurekebisha zaidi kwa usomaji wake wa mchezo.

**#4. Pedro Neto**

Pedro Neto amekuwa kwenye rada za Arsenal kwa muda mrefu sasa, na jina la Mreno huyo limeibuka tena. Tangu alipohamia Wolves mwaka wa 2019, Neto ameweza tu kuonesha mambo machache anayoweza kufanya kutokana na majeraha ya mara kwa mara yanayotatiza maendeleo yake. Hata hivyo, kiwango chake msimu huu hakijatambuliwa kabisa.

Licha ya kurejea hivi majuzi kutoka kwa jeraha lingine, Neto alikuwa mzuri mwanzoni mwa msimu, akitengeneza pasi nane za mabao kabla ya kuumia mwanzoni mwa Novemba. Alirejea uwanjani mwishoni mwa Desemba na kutengeneza asisti mbili zaidi katika Kombe la FA.

Neto anaweza kucheza kila upande wa winga, na atatoa kifuniko kinachohitajika, haswa upande wa kulia wa Bukayo Saka. Licha ya majeraha yake, Neto amejidhihirisha kuwa kwenye Ligi Kuu kwa miaka mitano iliyopita na atakuwa na nia ya kujidhihirisha katika klabu kubwa zaidi.

Huku Emile Smith Rowe akirejea tu kutoka kwenye jeraha na Reiss Nelson hakuna mahali popote katika mpango wa Arteta, kumsajili Neto katika majira ya joto bila shaka kutakuwa jambo la kuboresha. Nguvu ya Arsenal chini ya Arteta iko kwenye nafasi pana, na kuongeza mchezaji mwingine mwenye vipawa kwenye eneo hilo kutaimarisha kile ambacho timu yake inafanya vizuri zaidi.

**#5. Martin Zubimendi**

Mchezaji wa Real Sociedad, Martin Zubimendi, alihusishwa na kuhamia Arsenal mwanzoni mwa msimu huu, huku Washikabunduki wakiwa tayari kulipa kipengele chake cha kuruhusiwa kuondoka. Hata hivyo, Mhispania huyo alitaka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na klabu yake ya utotoni na akaamua kupinga hatua hiyo. Sasa, ikiwa ripoti zitaaminika, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anakaribia kujiunga na Arsenal katika makubaliano ya awali kabla ya msimu ujao.

Kwa majeraha ya Thomas Partey na kutokwenda sawa, Arsenal walitaka kuchukua nafasi yake katika majira ya joto yenyewe, na sasa kwa uwezekano wa Partey kuondoka msimu huu wa joto, na Zubimendi anaweza kuwa mbadala mzuri.

Zubimendi anacheza katikati ya safu, na utulivu wake, udhibiti, kuongoza mwelekeo wa uchezaji, na kuamuru mchezo kupoa, hizo ndio sifa zake kuu. Zubimendi ndiye chachu kati ya safu ya ulinzi na safu ya kati, na mara nyingi hujiweka kwenye mifuko ya nafasi ili kupokea pasi kati ya wachezaji wawili.

Ripoti zinaonesha Barcelona na Bayern Munich pia wana nia ya kumsajili, lakini Arteta amemshawishi kuhamia London Kaskazini. Baada ya kutumia fedha nyingi kwa Declan Rice msimu wa majira ya joto, Arsenal bado wanaonekana kukosa kitu katika safu ya kati, na Zubimendi anaweza kuwa jibu na anaweza kuwa mchezaji ambaye Partey alipaswa kuwa.

## Nukuu

"Manchester City wanacheza kwa kujiamini sana. Wana kikosi kizuri - wanaweza kubadilisha wachezaji watatu au wanne na bado washinde kwa urahisi. Je, ninawaona wakifanya makosa sawa na Liverpool na Arsenal? Ndiyo, naweza. Lakini wakati huo huo wengine wanaweza kufanya makosa kwa hivyo nadhani City wana faida kubwa," **Kocha wa zamani wa Liverpool na Real Madrid, Rafa Benitez, akiipa nafasi zaidi Manchester City katika mbio za ubingwa.**



"Siku zote imekuwa Lionel Messi," Arteta aliiambia Sky Sports (kupitia SPORTbible). "Kwa wanangu watatu, ni sawa kabisa. Tumekuwa na bahati sana kupata fursa ya kupata uzoefu wa mchezaji bora wa wakati wote. Kwangu mimi ndiye mkuu wa wakati wote," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akitoa jibu wazi alipoulizwa kuchagua kati ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi yupi bora zaidi.**



"Kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya PSG? Lilikuwa kosa langu. Nilipaswa kujizuia zaidi. Tulifanya makosa mengi dhidi ya PSG, nikiwamo mimi." **Kocha wa Barcelona, Xavi, akikiri kufanya makosa baada ya kutolewa Ligi ya Mabingwa Ulaya na PSG.**



"Kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya PSG? Lilikuwa kosa langu. Nilipaswa kujizuia zaidi. Tulifanya makosa mengi dhidi ya PSG, nikiwamo mimi." **Kocha wa Barcelona, Xavi, akikirui kufanya makosa baada ya kutolewa Ligi ya Mabingwa Ulaya na PSG.**



# KIBADENI KATIKA UFALME WAKE SIMBA VS YANGA

## ●● Atoa siri anayetaka kwa kuvunja rekodi yake ya hat-trick 'Dabi'...

**Na Saada Akida**

MIAKA 47 imepita tangu Abdallah 'King' Kibadeni, alipofunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mechi ya watani, 'Kariakoo Dabi', kati ya Simba na Yanga.

Hadi leo hii hakuna mchezaji yeyote si wa Simba au Yanga aliyefanya hivyo. Kibadeni akiwa amevaa jezi ya Simba namba 10, mgongoni akicheza nafasi hiyo, alifunga mabao matatu na kuiongoza timu yake kutoa kipigo kitakatifu cha mabao 6-0 kilichoingia kwenye historia ya 'dabi' na soka la Tanzania hadi leo hii.

Ilikuwa ni Julai 19, 1977 kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam (sasa Uhuru), alipoweka rekodi hiyo, akifunga mabao dakika ya 10, 42 na 89, mengine mawili yakifungwa na Jumanne Hassan 'Masimenti' dakika ya 60 na 73, huku beki wa Yanga, Selemani Sanga akijifunga mwenyewe dakika ya 20.

Mechi hiyo imebaki kwenye rekodi ya kuwa, Kibadeni ndiye binadamu wa kwanza kufunga 'hat-trick' katika mechi ya watani ambayo hadi leo hii miaka 47 imepita haijavunjwa.

Wapo wachezaji waliokaribia kufanya hivyo wakifunga mabao mawili kwenye 'dabi; kama Emmanuel Okwi, Hamis Kiiza, Jerry Tegete na hivi karibuni Max Nzengeli wa Yanga alitupia bao mbili, Novemba mwaka jana.

Kadiri miaka inavyozidi kusonga mbele haionekani dalili za kufikiwa au kuvunjwa kwa rekodi hiyo kutokana na idadi ndogo ya mabao ambayo yamekuwa yakifungwa na washambuliaji pindi timu hizo mbili kongwe zinapokutana.

Kitendawili kinabaki kuwa itachukua miaka mingapi hadi kuvunjwa kwa rekodi yake hiyo.

Mechi hiyo pia bado inasimama kuwa ndiyo mechi iliyotoa kipigo kikubwa zaidi katika mechi za 'dabi', mpaka sasa.

Nipashe limefika nyumbani kwa Kibadeni, Chanika jijini Dar es Salaam, na kuzungumza na mchezaji huyo wa zamani wa Simba na Timu ya taifa, Taifa Stars, ambaye jina lake halisi ni Abdallah Athumani Seif, lakini kutokana na umahiri wake kwenye soka mashabiki walimpachika majina mengine ambayo ni King Kibadeni Mputa', na kuongea naye juu ya mambo mbalimbali ya soka, tangu mchezaji hadi kuwa kocha.

King Kibadeni anaweka wazi mambo mbalimbali ikiwamo safari maisha yake ya sasa licha ya kutocheza, lakini anaishi katika soka akiwa na kituo chake cha KISA kilichopo katika mji wake huo.

### ATAKAYEMVUA UFALME WA HAT-TRICK

Kibadeni anasema bado anajivunia kwa miaka 47 sasa hakuna mtu ambaye amefanikiwa kufikia au kuvunja rekodi yake ya kufunga hat trick katika pambano la watani wa jadi.

"Watu wanatakiwa kukubali kuwa mimi bado ni mfalme, yeyote ambaye anataka kufikia au kuvunja rekodi yangu na kunipoka ufalme huu basi aje kwangu aniombe ni mpe baraka zangu.


"Atakayekuja kufuata baraka zangu basi tambua huyo ndiye atakayefikia na kuvunja rekodi hiyo iliyodumu takriban miaka 47 sasa tangu 1977," anasema Kibadeni.

### SABABU YA KUSHINDA BAO 6-0, 1977

"Unajua zamani tulikuwa tunaenda viwanjani kumuangalia mpinzani wetu tunayecheza naye hivi karibuni, nakumbuka kipindi hicho Simba tuliweka kambi Kibaha.

"Tukaenda Uwanja wa Karume, kuangalia Yanga inacheza na timu moja (hakumbuki jina), hiyo mechi walishinda bao 5-0, siku hiyo wachezaji wa Yanga walitozomea na kutumwagi michanga.

"Kitendo hicho kilituumiza sana, tukarudi kambini na tulipomaliza kula chakula cha usiku mida ya saa mbili, wachezaji wote tulifanya kikao chetu na kupanga mipango yetu," anasema.



King Kibadeni Mputa akikinoa kikosi chake cha Simba: **PICHA: MAKTABA**

Kibadeni anasema baada ya muda walikubaliana kila mchezaji mwenye gari alilipeleke uwanjani na kuwasha taa kwa ajili ya kupata mwanga na kuweza kufanya mazoezi usiku huo.

"Tulifanikiwa sana nakumbuka ilikuwa bado siku mbili kucheza na Yanga, tuliendelea kufanya mazoezi usiku huo, siku ya pili ilikuwa kazi ni hiyo dhamira yetu ni kuhakikisha tunalipa kisasi cha kumwagiwa michanga na kule kutuzomea," anaeleza mfalme huyo wa hat-trick katika mchezo wa Derby.

Anasema wachezaji wenzake walimuahidi kutengeneza nafasi na kazi yake kubwa kufunga, anakumbuka bao la sita katika mchezo huo pasi ya bao alipokea kutoka kwa Abbas Dilunga.

### FIGISU ZA MECHI NA YANGA 2013

"Hii ni mechi ambayo sitaisahau kwa sababu kulikuwa na mambo mengi nje ya uwanja, nakumbuka wakati tunajiandaa na mchezo huu tulienda kuweka kambi Kigamboni (Bamba Beach).

Kuna baadhi ya viongozi walikuja kwangu na kuniambia nisiruhusu kiongozi yeyote kuingia kambini kwa sababu walikuwa wakirubuni wachezaji," anasema.

Kibadeni anasema kwa kuwa viongozi hao waliniambia maneno hayo ndio hao walikuwa wakija kuzungumza na wachezaji akawa anapata wakati mgumu kwa sababu walifanya hivyo ili kuonekana uongozi haufai na wajiuzulu.

"Kabla ya mechi nilipewa majina ya wachezaji hao na niliwapanga kikosi cha kwanza lengo langu likiwa ni kuthibitisha niliyoambiwa.

Ni kweli maana hadi tunaenda mapumziko tayari tuko nyuma kwa mabao 3-0 nilikuwa katika hali mbaya sana.

Ila nilipoingia katika chumba cha kubadilisha nguo niliwaeleza wasaliti na kuwapa nafasi vijana wadogo kutoka kwenye timu yetu ya vinaja, akiwamo Galaxy (William Lucian), Jonas Mkude, Said Ndemla, Ramadhani Singano na wengine ," anaeleza Kibadeni.

Anasema aliwapa maelekezo madogo na kuwaamini wakafanye kile alichowapa kwenye uwanja wa mazoezi na kufanikiwa katika dakika 45 ya kipindi cha pili tukafanikiwa kusawazisha na waliwakosa kuwafunga bao la nne.

### KISA SIMBA AKOSA RAHA KWENYE MJI WAKE

"Hapa Chanika watu wote wananifahamu kuwa ni Simba, hivyo inapofanya vibaya nakosa amani na raha kwa sababu ya Simba wenzangu huja kuniuliza maswali mengi na wengine Yanga kunizodoa.

Hali hiyo ikanifanya niichukie kuangalia mpira na kuisusa Luninga na kutoangalia kabisa Simba kwa sababu ya kuepukana na maumivu hasa pale napoangalia na kufungwa," anasema kocha huyo.

### KUTOSHIRIKISHWA KWA NYOTA WA ZAMANI

Anaeleza kwamba licha ya wachezaji wa zamani kucheza kwa mafanikio, lakini wamewekwa nyuma na viongozi kwa kutopewa nafasi ya kutoa michango yao ikiwamo kupata nafasi ya kuzungumza na wachezaji, lakini kutoa mawazo juu ya timu yao.

"Unajua miaka ya sasa ni tofauti, zamani wachezaji tulikuwa tunajuana ukiharibu uwanjani unamfuata nyumbani kwake kumueleza. Sasa hivi tumekuwa na mchanganyiko wa wachezaji wazawa na wakigeni.

"Wakigeni wanakuja kwa ajili ya kazi mapenzi ya timu si sana, tofauti na wazawa hawa wanacheza kama kazi, lakini na mahaba, katika hilo kama wachezaji wa zamani inapofika mechi kubwa tunatakiwa kuzungumza nao kwa sababu kuna mambo mengi yanapita," anasema.

Kibadeni anasema kuna watu ambao wapo ndani ya Simba, lakini wanaumia timu inapofanya vizuri ba kufurahi inapoharibikiwa kipindi hicho ndicho cha kuweza kuzungumza na wachezaji kutorubuniwa.

### MFALME NDANI YA SIMBA SASA

Licha ya kiungo Clatous Chama kuimbwa kuwa ni mfalme wa Wekundu wa Msimbazi hao, lakini Kibadeni yuko tofauti na maono ya Wanasimba kwa kudai kwa sasa bado hajamuona mfalme ndani ya klabu hiyo.

"Chama ni mchezaji mzuri sana, lakini bado hajafikia ule ufalme niliokuwa nao kipindi changu, kwa sababu wachezaji wa sasa wanacheza mechi kwa vipindi, atakuonyesha mchezo mzuri mechi moja inayofuata hataonyesha kiwango kile," anasema nyota huyo wa zamani.

### SABABU YA KUPOTEA KWA SIMBA

Kibadeni anasema kuna mambo mengi hufanya timu hiyo kushindwa kuonyesha ubora wao wa misimu minne iliyopita ikiwamo kutokuwa wamoja.

"Ile kaulimbiu yetu ya 'Simba Nguvu Moja' haipo kwa sababu hatuko wamoja, baadhi ya watu waliopo ndani ya Simba, wanafurahi kuona timu inafanya vibaya, kwa mtindo huo ninaimani itakuwa ngumu kwetu kupata ubingwa kwa msimu huu," anahitimisha Kibadeni.

**JE, WAJUA?**



KATIKA mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu Ulaya mshambuliaji wa Bayern Munich, Harry Kane, ndiye anayeongoza kwenye Ligi Tano Bora barani humo akiwa na mabao 33, akifuatiwa na Serhou Guirassy (Stuttgart - 25), Kylian Mbappe (PSG - 24), Lautaro Martinez (Inter - 23), Lois Openda (RB Leipzig - 23).

# Serikali yasikia kilio wanandoa kutenganishwa mikoa ya kazi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imesia kilio cha wabunge cha kutaka watumishi wa serikali walio katika ndoa kutotenganishwa na wenza wao sehemu wanapofanya kazi, ikisema mwaka huu wa fedha watahakikisha wenza wanapohamishwa wanakwenda na wenza wao.

Akizungumza bungeni mwishoni mwa wiki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene alisema suala hilo litazingatiwa kwenye msawazo wa watumishi wa umma ambao wataufanya mwaka huu ikiwa ni hatua ya kukabiliana na upungufu wa watumishi.

"Kila mtumishi mwenye mwenza wa kweli atakwenda kufanya kazi mahali pamoja, siyo lazima kiwe kituo kimoja cha kazi kama ni walimu basi mmoja atafundisha shule hii na mwingine atafundisha shule hii.

Lakini mahali ambapo jioni wanakwenda kulala pamoja." "Ukiwa na cheti cha ndoa na umefunga ndoa ya kweli maana kuna ndoa nyingine za uongo uongo, hili hatuwezi kulikubali, tutahakikisha mwanya huu wa msawazo basi kila mtumishi tunawaunganisha ili waweze kufanya kazi kwa raha na starehe," alisema.

Alibainisha jambo hilo limekuwa likiwakera na wabunge wengi wamekuwa wakipeleka maombi katika ofisi yake na hatua hiyo itaongeza tija katika utendaji wa kazi.

Simbachawene alisema tatizo la upungufu wa watumishi katika baadhi ya maeneo inachangiwa na watumishi kurundikana katika baadhi ya maeneo.

Alisema: "Wabunge msirudi tena kulalamika kwa sababu tutakapoanza operesheni haitamwacha mtu na haitakuwa na upendeleo lakini tutazingatia hali na sababu mahususi waliyonayo watumishi".




Balozi wa Pakistani nchini, Siraj Ahmad Khan (kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Digit, Abdul Rehman Mahmood (katikati) na Mkurugenzi wa Biashara wa Vodacom Tanzania, Linda Riwa, wakipiga makofi wakati wa uzinduzi wa simu maalum iitwayo Smart Kitochi+, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa kuona na kusikia huku ikiongeza matumizi ya dijitali nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana wapigwa msasa namna ya kuomba fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUKWAA la Mabadiliko Tabianchi (Forum CC) limetoa mafunzo ya uandishi wa maandiko kwa vijana wanaojishughulisha na kilimo kwa ajili ya kuomba fedha za mapambano dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Fedha hizo ni Dola za Marekani milioni 200 ambazo zitatolewa na Shirika la GCF kwa kushirikiana na Benki ya CRDB nchini.

Ofisa programu wa Forum CC, Abdulaziz Mkwizu akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa juzi, alisema mafunzo hayo yanatokana na utafiti walioufanya kuhusu vikwazo walivyonavyo wakulima wadogo vijana kupata mitaji ya kuwekeza kwenye kilimo.

"Katika utafiti tuliofanya mwaka jana tulikuwa tunaangalia ni kwa namna gani vijana ambao ni wakulima wadogo wanaweza kunufaika na fedha hizi ambazo zinatolewa kwa ajili ya mapambano dhidi ya athari za mabadiliko tabia nchi" alisema Mkwizu.

Alisema katika utafiti huo moja ya vikwazo ambayo wameibaini ni kundi hilo kutokuwa na uwezo wa kuandika maandiko ambayo yatakuwa na sifa za kuwawezesha kupata fedha kwa ajili ya shughuli zao za kilimo.

"Vijana wengi hawana uwezo wa kuandika maandiko ambayo yatakidhi wao kuweza kuomba fedha, hivyo sisi kama Forum CC, tunatoa mafunzo haya ili kuwajengea uwezo wa kuweza kuandika maandiko ya kupata fedha hizo" alisema.

Aidha, alisema mafunzo hayo yanakuja kutokana na fursa ya fedha iliyopo hivi sasa ambapo Benki ya CRDB kwa kushirikiana na Shirika la GCF, wametoa fedha hizo.

"Hizi fedha vijana wanaojishughulisha na kilimo nchini watakiwa kuzikopa kupitia Benki ya CRDB lakini ili waweze kukopa wanatakiwa kuandika maandiko ambayo yatakubalika na kukidhi vigezo, ndiyo maana leo hii tupon-ao hapa kuwajengea uwezo" alisema Mkwizu.

Meneja miradi wa Shirika la Vijana la TAYOTA mkoani Tanga, Fatma Mkota, alisema vijana wengi wanashindwa kupata fedha kutoka taasisi mbalimbali za kifedha kunakosababishwa na kutokuwa na ujuzi wa kuandika maandiko.

Mkota alisema pamoja na uwepo wa fursa hizo za kifedha bado vijana wanakabiliwa na changamoto ya masharti ya mikopo ya fedha zinatolewa na mashirika mbalimbali ikiwemo riba kubwa pamoja na dhamana ya mkopo.

Alisema: "Tunaiomba serikali kuona ni kwa namna gani inaweza kutusaidia vijana kwakuwa bado hatuna ardhi wala kitu chochote cha kutusadia kuweka dhamana ya mkopo kwakua hata ardhi wengi wetu bado tunakodisha mashamba".

## Magonjwa ya mfumo wa hewa nchini bado tatizo

**Na Gwamaka Alipipi**

IDADI ya wagonjwa wanaofika kupata matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala kwa siku ni zaidi ya 500, huku idadi kubwa ni wale wanaosumbuliwa na magonjwa njia ya hewa.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala, Dk. Zavery Benela, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa utiaji saini mkataba wa makubaliano ya usambazaji majiko na mitungi ya gesi katika mikoa 10 kati ya Kampuni ya Oryx Gas na Taasisi ya Doris Mollel (DMF) iliyofanyika katika hospitali hiyo.

Kupitia mkataba huo, DMF itasambaza majiko na mitungi ya gesi ya oryx kwa wahudumu wa afya, hususani wanaofanya kazi katika mazingira magumu na wanaowahudumia wajawazito, mama na mtoto.

Akizungumza katia hafla hiyo, Dk. Benela alisema magonjwa ya mfumo wa hewa yanashika namba mbili kwa idadi ya wagonjwa nchini na kisababishi kikubwa ni hali ya hewa na mazingira ya kupikia.

"Endapo jamii ikiachana na matumizi ya kuni na mkaa katika kupika nina uhakika kwa asilimia kubwa tutapunguza ongezeko la magonjwa ya mfumo wa hewa. Mama akipika katika gesi inamsaidia kuepukana na kuvuta hewa chafu," alisema Dk. Benela.

Mkurugenzi wa DMF, Doris Mollel alisema wazo la kuwapatia wauguzi mitungi ya gesi na majiko walilibuni miaka mitatu iliyopita baada ya kwenda Mbagala kumtembea mama aliyejifungua watoto watatu ambao ni njiti.

"Tulipofika kwake tulikuta anaishi katika chumba kimoja, anapika hapo hapo tena kwa mkaa. Tukawaomba kampuni ya Oryx tuwape wazazi msaada wa majiko, mwaka jana tuliwafikia wajawazito 1,000," alisema Doris.

Doris alisema katika usambazaji wameanza na wahudumu wa afya katika hospitali hiyo kwa kutoa mitungi na majiko ya gesi 50, kwamba watawafikia watoa huduma za afya katika mikoa 10 Tanzania Bara na visiwani.

Alisema mwaka huu wameamua kuwafikia watoa huduma za afya ambao wanakutana na wagonjwa, hivyo itakuwa njia bora ya wao kwenda kuwaelimisha wagonjwa umuhimu wa kutumia nishati safi katika kupika.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Gesi ya Oryx Tanzania, Benoit Araman alisema wanajisikia furaha kuingia makubaliano na DMF katika usambazaji wa majiko na mitungi ya gesi mikoani.

Alisema kuna faida nyingi jamii inapata kutokana na matumizi ya gesi wakati wa kupika ikiwemo kulinda mazingira kunakotokana na jamii kuacha kukata miti.Alitaja faida nyingine ni inalinda afya kwa kinamama wakati wa kupika, inaokoa muda wa kupika pamoja na kumuokoa mtu kujeruhiwa na wanyama wakali pindi anapokwenda msituni kutafuta kuni.

Alisema hadi sasa kampuni yake imeshatoa mitungi ya gesi pamoja na majiko zaidi ya 10,000 katika taasisi mbalimbali na wajasiriamali.





# Utafiti: Asilimia 80 wakazi Mbeya wanakula katika migahawa

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

ASILIMIA 80 ya wakazi wa Jiji la Mbeya wamebainika wanakula vyakula vinavyoandaliwa kwenye migahawa, hali ambayo inaweza ikawasababishia magonjwa endapo watoa huduma wa migahawa hiyo hawatazingatia usalama wakati wa kuandaa.

Kutokana na hali hiyo, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanza kuwapatia mafunzo maalumu mama na babalishe kuhusu kuzingatia usalama wa chakula wanachouza, ili kuwaepusha wateja wao na magonjwa hasa ya mlipuko.

Takwimu hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja wa Mradi wa Kuboresha Lishe katika Majiji kutoka Shirika la HELVETAS, Agnes Mahembe wakati wa kutoa mafunzo hayo kwa watoa huduma hao.

HELVETAS ni miongoni mwa watekelezaji wa programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani (Agri- connect) hasa kwenye kipengele cha kuboresha lishe kwa jamii.

Alisema wengi wa wananchi hao wanakula chakula kinachoandaliwa kwenye migahawa kutokana na shughuli wanazofanya kuwa mbali na nyumbani.

"Lengo letu ni kuhakikisha wananchi wa Jiji hili wanapata lishe bora, wengi wanakula hotelini na kwenye migahawa kwahiyo tumeamua kukutana na hawa mamalishe na babalishe ili tuwape elimu ya namna ya kuzingatia usalama wa chakula," alisema Agnes.

Mkurugenzi wa Shirika la Chakula Tanzania, Ladislaus Nkomba alisema waliamua kutoa elimu hiyo ili kukidhi matakwa ya sheria za nchi na za kimataifa kuhusu usalama wa chakula kwa wananchi.

Alisema chakula kikiandaliwa kwenye mazingira ambayo usalama wake ni mdogo kuna hatari ya kutokea kwa magonjwa ya mlipuko ambayo yanaweza kugharimu maisha ya wananchi na kulisababishia taifa hasara.

Alisema wanawafundisha watoa huduma hao kwa kuwakusanya eneo moja na ili kupunguza gharama za kwenda kuwatembelea kwenye maeneo yao ya kazi.

Baadhi ya mama lishe na baba lishe ambao walihudhuria mafunzo hayo walisema kwenye maeneo yao ya kazi wamekuwa wakikabiliana na matatizo mbalimbali ikiwemo kuoneana wivu na kutoelewana hasa kuhusu usafi.

Mmoja wa watoa huduma hao, Efania William alisema asilimia kubwa ya maeneo wanayofanyia kazi ni kwenye masoko ambako kuna mikusanyiko mikubwa ya watu na hivyo kila mtoa huduma anakuwa na wateja wake.

Alisema ikitokea mmoja wa watoa huduma akawa anaandaa kwenye mazingira ambayo siyo rafiki wanaambizana lakini siyo wote wanakubali kutokana na kila mmoja kutokuwa na mafunzo.

"Tunawashukuru wataalamu hawa kwa kutupatia mafunzo haya, kule kwenye maeneo yetu ukimwambia mtu kwamba hapa hapafai kuandalia chakula huwa hatuelewani kwa sababu tu ya kuhisi pengine unamuonea wivu lakini kwa elimu hii naamini kila mmoja atakuwa mwalimu," alisema Efania.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alisema hivi karibuni ugonjwa wa kipindupindu ulilipuka katika baadhi ya maeneo nchini lakini hakuna hata kisa kimoja kilichoripotiwa katika Mkoa wa Mbeya.

Alisema elimu inayotolewa na wataalamu hao ikiendelea kuzingatiwa kuna uwezekano jiji hilo likaendelea kuwa salama zaidi hasa kuwafundisha watu kunawa mikono vizuri na kuandaa chakula kwenye maeneo safi.



Baadhi ya wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya, wakichota mchanga kwenye Mto Mbalizi hivi karibuni, kitendo kinachosababisha uharibifu wa mazingira na mto kuhama kwenye mkondo wake.
**PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waliokuwa wakisafirisha wagonjwa kwa machela wapewa 'ambulance'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imewapatia gari la kubeba wagonjwa wakazi wa Kata ya Makowo Halmashauri ya Mji Njombe, ambao awali walikuwa wakisafirisha wagonjwa na wajawazito kwenye pikipiki na machela za miti.

Wakizungumza wakati wa hafla ya kupokea gari hilo katika Kituo cha Afya Makoweo kilichopo Kijiji cha Makowo wananchi hao walisema ujio wa gari hilo ni ukombozi katika maisha yao.

Wamesema ujio wa gari hilo ni mkombozi kwa sababu walikuwa wakilazimika kutengeneza machela za miti za kubebea wagonjwa, huku wengine wakibeba wagonjwa kwenye bodaboda na kutembea umbali wa zaidi ya km 30 kufuata huduma za afya.

Mmoja wa wananchi hao akiwemo, Benedicto Mdete mkazi wa Kijiji cha Ng'elamo alisema kutokana na kukosekana gari la wagonjwa wajawazito walikuwa wanafariki dunia njiani wakiwa wanapelekwa kupata huduma.

Naye, Finanzia Haule alisema gari hilo ni msaada mkubwa kwa wananchi wa kata hiyo kwa sababu hapo mwanzo walikuwa wanakodi magari kwa gharama kubwa ili kufika kwenye vituo vya afya.

Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika aliwataka watumishi kutumia gari hiyo kwa kazi iliyokusudiwa na kuhoji endapo gari hiyo haitaonekana kituoni ama kutumika kinyume na kusudio la serikali. "Mkiona gari halionekani ulizeni maswali kwa sababu maeneo mengine tumeona kunakuwa na matumizi mabaya ya haya magari, msiogope pale mnapoona matumizi mabaya, tunzeni hili gari," alisema Mwanyika.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Dk. Jabir Juma alisema kazi ya serikali ni kusogeza huduma kwa wananchi na ndiyo maana imejenga kituo cha afya na sasa imepeleka gari la wagonjwa.

Askofu wa Jimbo Katoliki Njombe, Ausebius Kyando alishiriki katika hafla hiyo kwa kubariki kituo cha afya na gari la wagonjwa, huku akitoa rai kudhibitiwa kwa vifo visivyo vya lazima.

# Ardhi wilayani Rungwe yaanza kupimwa kupunguza migogoro

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

TUME ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, imeanza kupima ardhi na kupanga matumizi wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya ili kupunguza migogoro ya ardhi.

Upimaji huo ulianza kufanyika mwishoni mwa wiki katika Kata ya Suma wilayani hapa ambayo ni miongoni mwa wilaya zinazotajwa kuwa na migogoro mingi.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu alisema asilimia 90 ya kero za wananchi wilayani hapa ni migogoro ya ardhi inayotokana na maeneo mengi kutopimwa na kupangiwa matumizi.

Alisema baadhi ya migogoro hiyo ni ya wananchi wenyewe kwa wenyewe, wananchi na serikali na wananchi na baadhi ya wawekezaji na hivyo akaiomba tume kuendelea kupima ardhi kwenye vijiji vyote vya wilaya hiyo.

"Kwa mfano Halmashauri ya Busokelo ina vijiji 56 lakini hakuna hata kijiji kimoja ambacho kimepimwa na kupangiwa matumizi ya ardhi, sasa nawaomba wataalamu mtusaidie kuyapima maeneo yetu haya ili tuondokane na kero hii," alisema Haniu.

Alisema baadhi ya migogoro hiyo imekuwa ikichukua muda mrefu kutatuliwa kutokana na mazingira yake na hivyo kuchukua muda mrefu hali ambayo inakwamisha shughuli za maendeleo.

Meneja wa Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi ambayo iko chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo a Makazi, Pili Msati alisema waliamua kupima ardhi kwenye vijiji vya wilaya hiyo kutokana na kuwa na migogoro mingi.

Alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini hali ambayo pia inachochea ongezeko la migogoro kwa wananchi kugombea maeneo ya uzalishaji.

Alisema imani yao ni kwamba baada ya kukamilisha upimaji wa maeneo migogoro hiyo itakwisha kutokana na kila kipande cha ardhi kupangiwa matumizi.

"Ardhi ikipimwa na kupangiwa matumizi inapunguza kabisa migogoro kwa sababu kila kipande kinapangiwa matumizi na hakuna kuingiliana kwa matumizi, sasa hii wilaya migogoro mingi inayosuluhishwa ni ya ardhi ambayo sasa ni kero," alisema Pili.

Baadhi ya wananchi walisema upimaji huo wa ardhi utawasaidia kuondoa migogoro kwa maelezo kuwa wamekuwa wakishirikishwa katika kila hatua.



# Wasichana 100,000 kupatiwa chanjo ya saratani Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar inatarajia kutoa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi (HPV), kwa wasichana wenye umri kati ya miaka 9 -14 ili kuwalinda na ugonjwa huo.

Akizungumza jana visiwani hapa, Naibu Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya, Dk. Fatma Kabole alisema utoaji wa chanjo hiyo unatarajia kuwafikia watoto zaidi ya 100,000 katika shule za serikali na binafsi.

Aidha, alisema kumewekwa utaratibu maalumu wa kuwafikia watoto walioko nyumbani kupitia wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili kuweza kupata chanjo hiyo.

Alisema taakwimu zinaonesha kuwa saratani ya mlango wa kizazi inaongoza kuathiri wananwake, ambapo wananwake 466,000 wanagundulika na tatizo hilo kila mwaka, wengi wao wanatoka nchi zinazoendelea ikiwemo Zanzibar.

Hivyo, aliwataka walimu kusimamia chanjo hiyo sambamba na wazazi na walezi kutoa ushirikiano ili kufanikisha kazi hiyo.

Mratibu wa chanjo Kitengo Shirikishi Afya ya Uzazi na Mtoto, Abdulhamid Ameir Swaleh, aliwataka wazazi na walezi kupuuza taarifa potofu zinazotolewa na baadhi ya watu kuwa chanjo hiyo ina madhara.

Aidha, alisema chanjo hiyo ni salama na imeidhinishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Mamlaka ya Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA) kutumika kwa wasichana wenye umri wa kati ya miaka 9 hadi 14.

Utoaji wa chanjo dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi kutazinduliwa leo katika Shule ya Abeid Karume Micheweni Pemba na kuendelea hadi Aprili 25 katika shule za serikali, binafsi na katika ngazi ya jamii.

# Dk. Mwinyi: Serikali inathamini mchango wa wahandisi, wasanifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inathamini mchango wa fani za wasanifu, wahandisi na wakadiriaji kwenye utekelezaji wa mipango mikubwa ya maendeleo hasa miradi ya ujenzi.

Imesema itaendelea kuwahusisha kikamilifu kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji wa wataalamu wa kitanzania katika miradi endelevu ya kimkakati ya uwekezaji nchini.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi aliyasema hayo juzi wakati akizundua taasisi ya wasanifu, wahandisi na wakadiriaji Zanzibar.

Alisema serikali imejitahidi kuzitumia kampuni za ndani kwenye ujenzi wa miradi hasa wakati wa utekelezaji wa miradi mikubwa ya fedha za Uviko19 ambazo zilitumika kwa ndani kwa lengo la kuwajengea uwezo.

Dk. Mwinyi alisema serikali ya SMZ na SMT zinafanya jitihada za kushirikisha taaluma hizo kwenye shughuli tofauti za maendeleo, ikiwemo kuweka mazingira yanayowawezesha kujiajiri, kuhamasisha utambuzi wa fursa mbalimbali kupitia rasilimali zilizopo nchini pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya kufanikisha utafiti na ubunifu mbalimbali.

"Tunajua tunahitaji kushirikiana ili kufanikisha dhamira ya maendeleo endelevu hususani fani hizi kutokana na umuhimu wake kwa ustawi wa nchi yetu". alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, alisema serikali pia imefungua njia kwa fani hizo kuwa na uthubutu na kujiamini sambamba na kuwasihi wahandisi kuongeza juhudi ili kazi zao zizidi kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi.

Dk. Mwinyi alisema Tanzania ni nchi inayoendelea na inajivunia kufikia uchumi wa kati, kutokana na kuwa na miradi inayochangia zaidi pato la taifa, nyuma yake wakiwepo wenye fani za usanifu, uhandisi na ukadiriaji wa ujenzi.

Hata hivyo, alisema, Serikali ya Zanzibar kupitia uchumi wa buluu imeendeleza sera ya kuajiri wasanifu, wahandisi na wakadiriaji wazalendo, ikiamini kuna makandarasi wazuri na washauri elekezi mahiri wenye uwezo mkubwa wa kufanyakazi za uhandisi.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salim Mohamed alisema sekta ya majengo na ujenzi Zanzibar iko kwenye mageuzi makubwa.

Pia, alisema serikali inaendelea na ujenzi wa shule za ghorofa visiwani Unguja na Pemba, ujenzi wa hospitali kwa wilaya zote nchini, ujenzi wa nyumba za makazi, miundombinu ya maji safi na salama pamoja na umeme.

Alisema hatua hiyo inatokana na dhamira njema na maono ya Rais Mwinyi katika azma yake ya kuibadilisha Zanzibar.

Hivyo, alipongeza juhudi za wahandisi wote kwa ushiriki wa wao mkubwa wa mageuzi yanayoendelea nchini, chini ya uongozi wa Dk. Mwinyi, kupitia sekta ya ujenzi na miundombinu.

Rais wa Taasisi ya Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji Zanzibar, Abduswamad Mohamed Mattar alisema taasisi hiyo imedhamiria kufanya makubwa zaidi kama mchango wao kwa taifa na kuadhimia kuwa na wanachama wengi, kwamba kwa sasa kuna wanachama 192.



Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya wa Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Fatma Kabole akizungumza na waandishi wa habari mjini Unguja jana, kuhusu zoezi la chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana kati ya umri wa miaka 9-14, inayotarajiwa kuanza Aprili 22 hadi 25 mwaka huu nchi mzima. **PICHA: MAELEZO-ZNZ**

# Makamu wa Rais ahimiza utolewaji elimu ya kaboni kwa viongozi wakuu

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kuna umuhimu wa kujenga uelewa kwa viongozi wakuu wa serikali kuhusu usimamizi wa mwongozo wa kitaifa wa biashara ya kaboni, kwa ajili ya udhibiti na usimamizi bora wa biashara hiyo Zanzibar.

Aliyasema hayo jana katika hutuba yake iliyosomwa na Waziri wa Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salim Mohammed wakati wa ufunguzi wa semina ya kujenga uelewa kuhusu bishara ya kaboni kwa mawaziri, manaibu waziri na wakuu wa mikoa ya Zanzibar.

Alisema Zanzibar inaathirika na mabadiliko ya tabianchi kama vile mafuriko, ukame upepo mkali, mawimbi makubwa ya bahari na kusababisha kuongezeka kwa mmong'onyoko wa fukwe na kwamba biashara ya kaboni inahitajika katika kuikabili hali hiyo..

Aidha, alisema mambo hayo yanasababisha kuwepo athari kubwa ya kimazingira, kijamii na katika nyanya nyingine za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuathirika kwa biashara ya utalii , uvuvi, kilimo, ufugaji, upatikanaji wa maji ya chini ya aridhini na kuharibika kwa miundombinu.

Hivyo, alisema serikali ikifanya juhudi za kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ujenzi wa kuta, matuta, upandaji wa mikoko na miti na uhifadhi wa mazingira ya nchi kavu ya baharini.

Akizungunzia kuhusu upande wa Tanzania Bara kuhusu masuala ya biashara ya kaboni, Othman alisema suala hilo limeanza kuwekewa mwongozo na kwamba utatumika sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema Zanzibar kwa kuwa uchumi wake unaathirika na mabadiliko ya taibianchi ni wazi kwamba uanzishwaji na usimamizi bora wa biashara ya kaboni ni jambo linalohitajika.

Alisema uanzishwaji huko kutasaidia shughuli za upandaji miti , utunzaji na usimamizi wa miti, usimamizi wa taka, miundombinu ya usafiri ambayo hunufaisha watu wengi kwa wakati Mmoja.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dad Shajak, alisema kutokana na umuhimu wa kuendeleza biashara ya kaboni katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, serikali inaendelea na mchakato wa kutayarisha kanuni ili kuwepo mwongozo rasmi juu ya uendeshaji na usimamizi wa suala hilo.

Mratibu wa Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni, Profesa Eliakim Zahabu alisema kaboni ni biashara halisi na ikifanyika vyema inaweza kutoa tija kubwa kwa serikali na wananchi.

# Carbon First, Ruangwa watia saini makubaliano biashara hewa ukaa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Carbon First Tanzania Limited na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, zimetia saini hati ya makubaliano ya kufanya biashara ya hewa ukaa yenye lengo la kuwanufaisha wananchi wa wilaya hiyo na kutunza mazingira.

Tukio hilo lilifanyika juzi mjini Ruangwa na kushuhudiwa na Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo, wenyekiti na watendaji wa vijiji vitakavyohusishwa na mradi huo.

Kabla ya kusainiwa kwa mkataba huo, Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa walifanya kikao maalum cha kujadili makubaliano hayo na kuridhia na kuipa baraka zote halmashauri hiyo kusaini mkataba huo.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo wa kufanya biashara hiyo ya hewa ukaa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Andrew Chikongwe, aliwashukuru madiwani kwa kuridhia kusainiwa kwa mkataba huo. Chikongwe alisema tukio hilo lina maana ya kuwakaribisha wawekezeshaji hao kuanza kufanya taratibu nyingine za kutekeleza mradi huo wenye lengo la kutunza mazingira ikiwa sambamba na kuinua kipato cha wananchi wa Ruangwa.

"Tukio la leo ni zao la safari ya mafunzo kuhusu biashara hii tuliyoifanya katika halmashauri ya Tanganyika mkoani Katavi, tunaishukuru sana Carbon First kwa kukubali kushirikiana na sisi katika kutekeleza mradi huu wa hewa ukaa," alisema Chikongwe.

Alisema mradi huo ni mpya, na baada ya kuwakaribisha hatua ya kwanza ni kutoa elimu kwa wananchi wa vijiji 14 ambavyo vitahusika na mradi huo ili kujenga uelewa wa kutosha kabla ya kuanza kwa mradi huo.

Ofisa Mkuu wa Operesheni wa Carbon First Tanzania Ltd, Iftikhar Khan, ameishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa kuwakaribisha na amewaahidi mradi huo unaenda kubadilisha jamii nzima ya maeneo hayo.

Khan alisema baada ya kusaini hati ya makubaliano watafuata hatua nyingine kwa haraka ili wasaini mkataba kamili wa biashara hiyo kwa lengo la kutimiza azma ya mradi huo kuinua jamii kiuchumi na kutunza mazingira.

Mtaalam Mshauri wa Mazingira wa Carbon First Tanzania Ltd, Injinia Elisekile Mbwile, alisema mradi utaokoa misitu kwa kubadilisha kipato cha ukaa na mbao kugeukia hewa ukaa.

"Takwimu zinaonesha heka 400,000 zinaharibiwa ndani ya mwaka mmoja, lakini kupitia mradi huu unakwenda kuokoa misitu hiyo, kwani mwananchi badala ya kufikiria kukata mbao au mkaa, atatunza misitu ili kupata faida ya biashara ya hewa ukaa," alisema.

Injia Elisekile alisema pia watakwenda kukagua aina ya miti katika misitu hiyo, umri wa miti hiyo na udongo wa maeneo husika kwa lengo la kuona uwezekano wa kupanda miti mingine.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Frank Chonya, alisema jumla ya hekta 250,000 kutoka katika vijiji 14 zitatumiwa katika mradi huo ambao wamejipanga uanze haraka iwezekano ili utoe matunda kwa wananchi wa Ruangwa.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, ambaye ni Katibu Tawala wa halmashauri hiyo, Mhandisi Zainab Rashid, aliishukuru kampuni ya Carbon First Tanzania Ltd kwa kuichagua Ruangwa kutekeleza mradi huo ambao unakwenda kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja.



Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Prof. Tandi Lwoga (kulia) akimkabidhi tuzo mgeni Rasm, Edward Talawa ambaye ni Mkurugenzi mkuu wa FINCA Microfinance Bank kwa kushiriki siku ya Atamizi (Incubation) mwishoni mwa wiki na kufungua milango kwa CBE kushirikiana na FINCA Microfinance Benki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wajasiriamali wanawake wakumbushwa viwango

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI wanawake Mkoa wa Pwani wanachama wa Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake (TWCC), wametakiwa kuzingatia ubora wa bidhaa zao ili kuingia katika ushindani wa Soko Huru la Afrika (AFCFTA).

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwanasheria wa Halmashauri ya Bagamoyo, Hemedi Malogo, wakati akifunga mafunzo ya siku mbili yaliyoandaliwa na TWCC wilayani Bagamoyo.

Alisema bidhaa zenye ubora huongeza thamani ya bidhaa na kukabiliana na ushindani sokoni, aliwataka wanawake hao kuangalia pia fursa kwenye masoko ya nje ya nchi.

Alisema wajasiriamali wa Mkoa wa Pwani wanaweza kutumia fursa ya mazao yanayopatikana mkoani humo kwa kuyaongezea thamani ili kujiongezea kipato.

Mkoa wa Pwani una bidhaa za Kilimo, Mifugo, Uvuvi, pamoja na ufugaji, vyote vikitumiwa vizuri vinaweza kukuza pato la mtu mmoja mmoja, familia na hatimaye taifa.

Alisema serikali imeweka kipaumbele kuwawezesha wajasiriamali wanawake na vijana na mikopo mbalimbali imekuwa ikitolewa kama sehemu ya kuwainua.

Alisema Tanzania ni mwanachama wa jumuiya mbalimbali za maendeleo ya kikanda na kimataifa ikiwamo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na imeridhia utekelezaji Mkataba wa eneo la Soko Huru la Afrika (AFCFTA) ili kutoa fursa za masoko kwa Watanzania.

Alisema ni matumaini ya serikali kuona wajasiriamali wanazitumia vizuri fursa hizo ili waweze kunufaika nazo kwa kuwa Tanzania inazalisha bidhaa nyingi zenye ubora na wanawake wanatakiwa wawe mstari wa mbele kuchangamkia fursa.

Alizitaka taasisi mbalimbali za serikali ambazo zimeshiriki kwenye mafunzo hayo, kushirikiana na wafanyabiashara hao ili bidhaa zao zifuate taratibu na kanuni zote ili zikue na kuwa endelevu.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TWCC, Mercy Sila, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wafanyabiashara wanawake kuhusu taratibu, sheria na kanuni za kufanya biashara kwenye maeneo waliyopo na kwenye soko la Afrika (AFCFTA).

Alisema kupitia TWCC wanawake wanaweza kupiga hatua kimaendeleo kwenye biashara zao na kujua njia mbalimbali za kukuza mitaji, kuboresha biashara na kutafuta masoko.

Aliishukuru serikali kupitia Rais Samia kwa kutoa umuhimu kwa wanawake na kuwatengea mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya halmashauri ili kujiendeleza kupitia vikundi vyao.

Nao washiriki wa mafunzo hayo waliishukuru TWCC kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo walisema yamewajengea uelewa mkubwa katika masuala mbalimbali yanayohusu biashara.

Amina Abdul, alisema kupitia mafunzo hayo wamepata uelewa kuhusu ulipaji kodi, uelewa wa kupata kusajili majina ya Kampuni, kupitia taasisi na mashirika yaliyokuwapo kwenye mafunzo hayo.

Taasisi na mashirika yaliyoshiriki mafunzo hayo kwa lengo ka kutoa elimu ni Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) Shirika la Viwango (TBS), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na TWCC, yamewashirikisha wafanyabiashara wanawake wa Mkoa wa Pwani kutoka Halmashauri za Bagamoyo, Chalinze, Kibaha, Mkuranga, Kibiti na Mafia.

# Msajili Mahakama abaini mambo 43 kufanyiwa kazi

**Na Grace Gurisha**

MSAJILI Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Eva Nkya, amesema amepitia ripoti na kuona kuna mambo 43 ambayo anatakiwa kuyafanyia kazi.

Nkya aliapishwa Aprili 4, mwaka huu na Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kukabidhiwa ofisi juzi na aliyekuwa Msajili Mkuu wa Mahakama Tanzania, Wilbert Chuma.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, ameahidi kutekeleza majukumu yake na kuomba ushirikiano kutoka kwa wafanyakazi na wadau wa mahakama ili kuyatimiza kwa wakati.

"Nilivyopitia ripoti haraka niliona kuna mambo 43 ambayo ninatakiwa kuyafanya kwa hiyo, ninaomba ushirikiano mkubwa ili kutimiza hayo."

Aliahidi kutekeleza mikakati iliyowekwa na mahakama kwa ajili ya utoaji haki.

"Msingi mkubwa nitahitaji ushirikiano kwa majaji. Nikiwapigia simu ninaomba mnisaidie, kama kitengo cha maboresho ni muhimu sana, kwa hiyo nitawasumbua na pia, sheria inatulazimisha kushirikiana kati ya Msajili wa Mahakama na Mtendaji Mkuu wa Mahakama," alikumbusha.

Chuma alisema mrundikano wa mashauri ya mahakama umepungua kutoka asilimia 11 kwa mwaka 2019 hadi asilimia tatu, mwezi Machi, 2024.

Alisema hiyo ni mikakati ya mahakama kuendelea kusimamia na kusaidia kuondokana na mrundikano huo ambao pia, ni mafanikio ya mahakama na Nkya anatakiwa kuyaendeleza.

Chuma alisema Msajili huyo anatakiwa kuendelea kusimamia Mfumo wa Uratibu wa Mashauri (Advanced Case Management System), kusimamia na kuratibu Mfumo wa Unukuzi na Tafsiri (Transcription and Translation System (TTs).

"Kuhakikisha uamuzi wa Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu unapatikana katika mfumo wa TANZLII. Kutoka mwaka 2018 hadi sasa, jumla ya maamuzi 50,505 yamepandishwa kwenye mfumo," alisema Chuma.

Alisema idadi ya vituo vya mahakama vinavyokaguliwa vimeongezeka kutoka asilimia 75.8 mwaka 2017 hadi asilimia 98 mwaka 2023.

Aidha, utekelezaji wa maoni kuhusu ripoti ya REPOA ya mwaka 2023 ambayo kuridhika kwa umma kuhusu huduma zinazotolewa na mahakama, iliongezeka kutoka asilimia asilimia 61 ya mwaka 2015 hadi asilimia 88, mwaka 2023.

## Daktari ashauri maandalizi kubeba ujauzito

**Na Christina Mwakangale**

DAKTARI Bingwa Mbobezi wa Uzazi kwa Wanawake katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)- Tawi la Mlogamzila, Dk. Isaac Rugemalila, amewashauri wanawake kufanya maandalizi miezi mitatu kabla ya kubeba ujauzito, ili kuzaa watoto wasio na kasoro.

Amesema kasoro za kiafya zinazoweza kutokea kama hakuna maandalizi ni pamoja na kuzaliwa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi. Amesema yanaweza kuepukwa iwapo mwanamke atakuwa na madini chuma mwilini au kuzingatia ulaji ndizi mbivu.

Bingwa huyo akizungumza na Nipashe wiki hii, Dar es Salaam, alisema tatizo hilo husababishwa na mwanamke katika siku 21 hadi 28 za kwanza za ukuaji mimba na si ubora duni wa mbegu ya kiume inayotungusha mimba.

"Kwa wenzetu (nchi zilizoendelea), wenza huwa wanatembelea madaktari bingwa wa wanawake na uzazi kujiandaa kushika ujauzito. Tofauti tuliyo nayo kwetu sisi (nchi zinazoendelea) ujauzito unapatikana kwa dharura.

"Mara nyingi maandalizi utayakuta kwa wanaokwenda kupandikiza ujauzito (IVF) na wengi wao kiwango cha kuzaa watoto wenye mgongo wazi ni nadra kwa sababu wanakuwa wamejiandaa. Ni vizuri mama akajiandaa kabla ya uzazi," alisema Dk. Rugemalila.

Alisema tatizo hilo, ambalo huanza ndani ya wiki tatu au nne za awali wakati wa uundwaji wa kiumbe tumboni, na kwamba katika kliniki hospitalini hapo, ni nadra kumhudumia mwanamke aliyefika kupata huduma ya kujiandaa kushika ujauzito.

"Mama akiwa na 'follic acid' maana yake wake mfumo wa uti wa mgongo unapojitengeneza itasaidia mtoto asiwe na tatizo hilo. Wengi wanaofika kliniki tayari ni wajawazito, ni nadra afike hana ujauzito, zaidi kama hana, amekuja hapa akiwa na shida ya kubeba mimba ndio atakutana na ushauri.

"Mtoto kuzaliwa na tatizo la kichwa kikubwa kwa asilimia kubwa hutokana na matatizo ya vinasaba, kama mama atawahi mapema kwa daktari bingwa wa afya ya uzazi atapatiwa ushauri utakaosaidia ukuaji wa mtoto wakati akiwa tumboni mwa mama" alisema.

Alibainisha kwamba mwanamke akifika hospitalini mapema, atapatiwa ushauri na kupewa dawa muhimu zitakazosaidia ukuaji wa mtoto akiwa tumboni mwa mama yake, anapohudhuria kliniki.

"Kuna nchi nyingine sera zao ni lazima, mama kujiandaa. Lakini hapa wengi kutokana na mazingira yetu nafaka nyingi zinatoka shambani tunakula, kabla ya pengine kwenda viwandani na kuongezwa virutubisho.

# SGR yaanza rasmi safari majaribio Dar -Dodoma

**Frank Monyo na Pilly Kigome**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amezindua safari ya kwanza ya majaribio treni ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ikiwa ni sehemu ya maendeleo yaliyopatikana kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana katika uzinduzi wa safari hiyo, alisema kuzinduliwa safari hiyo ni mafanikio ya miaka 60 ya Muungano ikiwa ni tukio la kwanza la kitaifa kwa ukubwa wake ambalo limeudhuliwa na viongozi wa madhehebu yote nchini.

Alisema viongozi wa dini wamekuwa na umuhimu mkubwa katika safari hiyo kwa kuwa nchi ina thamini dini na ndio maana inaendelea kushirikiana na viongozi wa dini zote na kutoa uhuru kwa Watanzania kushiriki kulingana na dini zao.

Alifafanua kuwa Tanzania hadi kufikia hapo inatokana na mchango wa viongozi kuendeleza tunu za nchi inayotokana na Watanzania kuwa na imani za kidini ambazo wamebobea katika eneo hilo na kuwapa kipawa cha kusimamia amani.

"Kwa umuhimu wenu hata kesho (keshokutwa) nyinyi ni watu muhimu katika dua kubwa ya kuliombea taifa letu dua litakalofanyika mkoani Dodoma, viongozi wa dini mnaliheshimisha taifa letu kwa kujiandalia utaratibu wenu wa kukutana pamoja kwa imani tofauti bila kuleta tofauti yoyote "

"Tanzania ni nchi iliyoteuliwa na Mungu kwa imani yake na utulivu wake na kuwa na viongozi wenye karama kwa kuleta utulivu huo," alisisitiza.

Aidha, alisema Tanzania iko katika wiki ya maadhimisho ya miaka 60 ya ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kunakuwa na shughuli mbalimbali za maendeleo ndani ya nchi ikiwamo kuzindua miradi, kuweka mawe ya msingi, kufanya makongamano mbalimbali ya kuelimisha wananchi na kutoa nafasi ya kueleza Muungano ulivyoanzishwa mpaka kazi zilizofanywa na viongozi walioanzisha.

Mkurugenzi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa alisema awamu ya kwanza ya ujenzi wa SGR una kilomita 1,596 ndani yake kilomita 1,219 ni za njia kuu, ujenzi unatekelezwa kwa vipande vitano umbali wa kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro.

Kipande cha pili kiko asilimia 96.61 njia yote imeshakamilikama kuna baadhi ya vitu vichache vidogo havijaamalizwa lakini kwamaana ya njia imeshakamilika.

Kipande cha tatu kiko asilimia 14.22 kutoka Makotopola ya Singida kwenda Tabora na kipande cha nne kiko asilimia sita na cha tano kutoka Isaka Mwanza kiko aslimia 56.21.

Alisema TRC inaendelea kufanya majaribio ya treni ya kisasa katika kipande cha Dar esalaam Dodoma ikiwa ni maandalizi ya kuelekea Julai kwakuwa Rais Samia Suluhu Hassan kutoa agizo hadi ifikapo mwishoni mwa mwezi Julai iwe tayari imeshaanza.

Hadi sasa tayari TRC hadi kufikia mwezi Aprili wameshapokea mabehewa 65, seti moja ya kisasa inayotumia nishati ya umeme ya kichwa mchongoko na tayari vichwa tisa vimeshafika jumla vinahitajika 17.

Alifafanua reli hii SGR ni muhimili mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa taifa na kuchangiza mapinduzi ya sekta ya viwanda kilimo, ujenzi ufugaji, usafarishaji na madini.

Alisema Safari ya uzinduzi wa kwanza Dar es Salaam Dodoma itachukua saa tatu.

Naibu Waziri Wizara ya Uchukuzi, David Kihenzile alisema wanaendelea kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha ifikapo Julai huduma za usafiri huo zinaanza.

Alisema sasa wako katika mazungumzo ya ujenzi wa reli kutoka Dar esSalaam hadi Uganda wa kilomita 1860



Mkurugenzi wa Taasisi ya Doris Mollel Foundation, Doris Mollel (katikati) akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakati wa utiaji saini makubaliano ya ushirikiano kati ya taasisi hiyo na Kampuni ya Oryx Gas Tanzania kwa ajili ya kugawa mitungi ya gesi kwa wauguzi wa hospitali mbalimbali nchini. Kulia ni Mkurugenzi wa Oryx, Benoit Araman na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwananyamala, Zavery Benela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Ndejembi atoa hakikisho watumishi wanaoumia kazini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Deogratius Ndejembi amewahakikishia majaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi na wadau wengine kuwa, serikali inayachukulia kwa uzito maoni yao kuhusu kuboresha baadhi ya vifungu vya sheria ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia, kuugua ama kufariki kutokana na kazi.

Kiongozi huyo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifungua kikao kazi kati ya majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania-Divisheni ya Kazi, Kanda ya Kati ya Magharibi, Kamishna wa Kazi, Menejimenti ya Mfuko wa Fidia Kwa Wafanyakazi na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Aprili 20, 2024 mkoani Kigoma.

"Tayari maoni mliyotoa ya kuboresha kifungu cha 39 (2) cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi (Sura 263] kilichoweka ukomo wa muda wa kuwasilisha madai bila kutoa wigo wa kupokea madai hayo iwapo kuna sababu za msingi za kucheleweshwa kwake, tumeshayafanyia kazi na maboresho hayo kuwa sehemu ya muswada wa marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii uliosomwa bungeni kwa mara ya kwanza Februari 15, mwaka huu," alifafanua.

Aidha, Ndejembi alisema WCF kwa kushirikiana na Kurugenzi ya Hifadhi ya Jamii Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), wanaendelea na uchambuzi wa maboresho ya sheria ya fidia kwa wafanyakazi iliyotolewa na majaji hao.

Awali, akifungua kikao hicho Aprili 19, 2024, Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, alisema Katiba inasema "Lengo la vyombo vyote vya dola ni ustawi wa wananchi, WCF kama chombo cha serikali inagusa ustawi wa wananchi."

Aidha, Profesa Juma alihimiza umakini na uadilifu katika utekelezaji wa sheria hiyo ya fidia kwa wafanyakazi.

Jaji Mkuu ameipongeza WCF kwa kupiga hatua kubwa katika matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yake na kukumbusha umuhimu wa mifumo ya taasisi za umma kusomana ili kurahisisha utoaji wa huduma.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini WCF, Emmanuel Humba, amesema wataendelea kushirikiana na mahakama na kwamba pamoja na kwamba jukumu la kulipa fidia limekasimiwa kwenye mfuko, sheria imeweka utaratibu na vyombo vya kushughulikia madai ya wanufaika pale wanapokuwa hawajaridhika na fidia iliyolipwa au maamuzi ya Mfuko yanayokinzana na matarajio yao.

Mkurugenzi Mkuu WCF, Dk. John Mduma alisema ushirikiano baina ya mfuko na mahakama ni muhimu kwa vile kuna maeneo mengi ambayo mfuko unakutana na mahakama katika utekelezaji wa majukumu yake.

"Sisi kama WCF shughuli zetu hazikamiliki bila ya uwepo wa shughuli za mahakama. kwa mfano katika kushughulikia masuala yanayohusu mirathi, mfuko hutegemea maamuzi ya mahakama." alisema Dk. Mduma.

HABARI MICHEZO

# MASHABIKI MTOKO WA KIBINGWA WAKOSHWA NA MECHI YA WATANI

**Mwandishi Wetu**

WAKATI mashabiki wa Yanga wakiendelea kutamba baada ya ushindi wa mabao 2-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, dhidi ya watani zao Simba, mabingwa wa 'Mtoko wa Kibingwa' wameizungumzia dabi hiyo huku wale wanazi wa timu iliyoshinda wakisema walistahili pointi tatu.

Mabingwa hao ni kati ya 56 waliopata fursa ya kuishuhudia dabi hiyo kwa hadhi ya VIP kwa gharama za Kampuni ya Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Betika katika msimu wa saba wa kampeni ya Mtoko wa Kibingwa.

Mabingwa hao kutoka mikoa mbalimbali nchini kwa nyakati tofauti walisema kwao haijawahi kutokea.

Wale wanazi wa Yanga, waliishukuru Betika kwa kuwapa fursa ya kuishuhudia dabi hiyo laivu wakijinasibu kwamba imewasogeza karibu na ubingwa.

Uria Mtalika wa Kaliua Tabora, alisema imekuwa dabi ya kihistoria kwake, kwanza kuishuhudia kwa hadhi ya VIP na Yanga kutwaa pointi tatu, ambazo zimeisogeza kwenye ubingwa.

Clinton Festo wa Kigoma alisema Yanga na Betika wameongeza kitu kwenye maisha yake ya mpira.

**"Nimeishuhudia timu yangu (Yanga) ikicheza kwa kiwango cha hali ya juu, tena nikiwa VIP ni jambo ambalo sikuwahi kulitarajia, lakini Betika imenipa fursa hiyo," alisema.**

Mashabiki wa Simba, Kimara Mapunda wa Sumbawanga na Musa John wa Arusha waliwapongeza wale wa Yanga kwa kusema katika mechi kuna kushinda na kushindwa.

Kabla ya mechi hiyo, Ijumaa usiku mashabiki hao walishiriki burudani ya 'Bata la Mtoko wa Kibingwa' kwenye viwanja vya Mbagala Zakhem iliyoongozwa na wasanii, Chino Wanaman, Sholo Mwamba na Mzee wa Bwax.

Balozi wa kampeni hiyo, msimu huu, Baraka Mpenja, amesema mabingwa hao ambao ni wale wa mkoani waliondoka jana kwa ndege ni washindi wa kampeni ya Mtoko wa Kibingwa inayofanywa na Betika kila mwaka.

Ofisa Habari wa Betika, Juvelinaus Rugambwa, alisema kama kawaida yao, hawana mbambamba na msimu huu waliongeza idadi ya mabingwa hadi kufikia 56 ambao ni miongoni mwa waliobeti kwa kuandika Betika

"Baada ya dabi, mashabiki wetu wakae mkao wa kula hapa ni bandika bandua, Betika hatuna mbambamba," alisema.




Baadhi ya mashabiki waliondisha Kampeni ya 'Mtoko wa Kibingwa', wakifurahia burudani ya 'Bata la Mtoko' kabla ya kwenda kuishuhudia Dabi ya Kariakoo juzi kati ya Simba na Yanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kocha Azam: Si rahisi kushinda zote

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Azam FC, Youssoph Dabo, amebainisha kuwa kutoka na ugumu wa Ligi Kuu Tanzania Bara si rahisi kushinda kila mechi.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, kocha huyo alisema timu yake inapopoteza au kutoka sare kunakuwa na maneno mengi kana kwamba klabu imeundwa ili iwe inashinda mechi zote kitu ambacho hakiwezekani kwa klabu yoyote ya mpira wa miguu duniani.

"Tulishinda dhidi ya Namungo haikuwa shida, lakini tulipotoa suluhu dhidi ya Mashujaa FC maneno mengi yakaanza, hii ni ligi, tunapambana, kila mpinzani yupo kwenye kiwango bora, timu zinasaka ubingwa na wengine kuepuka kushuka daraja. Si rahisi kushinda mechi zote, tuna uwezo wa kumfunga kila mpinzani anayekuja mbele yetu, lakini wakati mwingine tukubali kwamba si lazima kushinda mechi zote," alisema kocha huyo raia wa Senegal.

Baada ya kuifunga Namungo mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi, Aprili 14, mwaka huu, ilitegemewa kuifunga Mashujaa FC mechi iliyochezwa, Uwanja wa Azam Complex, lakini ikalazimishwa suluhu kitu ambacho kilizua maswali na maneno mengi kutoka kwa mashabiki wa soka.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hasheem Ibwe, amesema bado wanaona wana nafasi ya kutwaa ubingwa msimu huu kwa sababu mahesabu yanawabeba.

"Tumekuwa tukibezwa tukipata matokeo yasiyoridhisha, wala si dhambi kwa sababu wapinzani wetu nao huwa wanakuja kusaka ushindi kama sisi, yanayotokea ni moja kati ya matokeo ya mchezo wa mpira wa miguu, hatuhuzuniki, tunachofanya tunasonga mbele kuangalia mechi zinazofuata, njia ya ubingwa haijazibwa, bado ipo, hatujakata tamaa, hatujanyoosha mikono kwa sababu wenzetu wanashinda, hili ni soka lolote linaweza kutokea," alisema Ibwe ambaye timu yake jana usiku ilitarajiwa kucheza dhidi ya Ihefu FC.

# Beno agomea wito Singida FG

**Na Shufaa Lyimo**

MLINDA mlango wa Klabu ya Singida Fountain Gate, Beno Kakolanya, amegoma kuhudhuria kikao cha Kamati ya Utendaji akidai hakitamtendea haki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Msemaji wa timu hiyo, Hussein Masanza, alisema mlinda mlango huyo aliandikiwa barua ya wito Aprili 15, ikimtaka kuhudhuria kikao cha Kamati ya Nidhamu Aprili 19, mwaka huu, lakini alishindwa kutii wito huo.

„Ni kweli Beno alipewa barua ya wito na Kamati ya Nidhamu ikimtaka ahudhurie kikao ambacho kilipangwa kufanyika Aprili 19, lakini aligoma akidai kamati haitamtendea haki kutokana na tuhuma alizotuhumiwa za kuihujumu timu yao," alisema Masanza.

Alisema alipaswa kwenda kujibu sababu zilizomfanya atoroke kambini na kuhujumu timu yao hiyo siku chache kabla ya kukutana na timu ya Yanga katika mchezo ambao ulichezwa Aprili 14, mwaka huu jijini Mwanza.

Aliongeza kuwa kwa kitendo alichokifanya uongozi utamchukulia hatua kali ili iwe fundisho kwa kuwa ameonyesha utovu wa nidhamu.

Nipashe lilipomtafuta Beno kupitia simu yake ya mkononi ili kujua kwa nini hakuitikia wito huo, hakupatikana hewani.

# Jang'ombe yainyoa Kundemba FA Cup

**Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KIWEMBE cha 'Wakombozi wa Ng'ambo' Taifa Jang'ombe FC kimefanikiwa kuwakata Vigogo wa Ligi Kuu ya Zanzibar Kundemba FC katika michuano ya Kombe la FA.

Katika mchezo huo uliopigwa juzi, hadi dakika 90 zinakamilika zilikuwa timu hizo zilikuwa zimetoshana nguvu kwa bao 1-1, ambapo changamoto ya mikwaju ya penalti ilichukua nafasi yake na Kundemba kuondolewa kwa mikwaju ya penalti 4-5, mchezo uliochezwa Uwanja wa Mau A.

Kocha Msaidizi wa Taifa Jang'ombe, Othman Bariki, akizungumza na gazeti hili baada ya kumalizika mchezo huo, alisema anawapongeza wachezaji wake kwa mchezo mzuri walioucheza mpaka kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali.

Alisema wamecheza na timu kubwa kutoka Ligi Kuu ya Zanzibar, lakini wachezaji wake walicheza kwa utulivu ili kutimiza lengo lao la kuhakikisha wanasonga mbele.

"Tumecheza kwa kuwaheshimu wapinzani wetu, tunajua Tumecheza na timu kubwa na yenye hamasa, wachezaji walijituma hata tulipotangulia kufungwa hawakurudi nyuma,"alisema.

Kwa upande wa Meneja wa timu ya Kundemba FC, Nassor Mzaka, alisema sasa wanaenda kujipanga kuelekea michezo ya Ligi Kuu.

Alisema lengo lao la kufika fainali katika michuano hiyo halikufanikiwa hivyo nguvu zao wanazielekeza katika michezo kumi ya Ligi iliyobaki.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**SILVA KWENYE RADA MADRID**

REAL Madrid inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva, 29. (*Star*)

**PALMER NA WEST HAM**

KLABU ya West Ham ilikuwa na mpango wa kumsajili mshambuliaji wa England, Cole Palmer mwenye umri wa miaka 21, kutoka Manchester City kabla ya Chelsea kumnunua msimu uliopita. (*Sun*)

**GRIEZMAN MKATABA MPYA**

KLABU ya Atletico Madrid inapania kumpa mkataba mpya mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 33, huku ule wa sasa ukikamilika 2026. (*Rudy Galetti*)

**GIMENEZ AWINDWA ARSENAL**

ARSENAL, Juventus na Atletico Madrid zinawaniwa kumsajili mshambuliaji wa Mexico, Santiago Gimenez mwenye umri wa miaka 23, ambaye yuko tayari kuondoka Feyenoord ya Uholanzi. (*Mail*)

**OLMO KUREJESHWA BARCA**

BARCELONA inatamani kumrejesha mchezaji wao wa zamani wa akademi, Dani Olmo mwenye umri wa miaka 25, kutoka RB Leipzig. Mshambuliaji huyo wa Hispania ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 60 katika mkataba wake. (*Mundo Deportivo*)

**HUMMELS KUONGEZEWA**

KLABU ya Borussia Dortmund ipo kwenye „mazungumzo“ ya kuongeza mkataba wa beki wa kati wa Ujerumani, Mats Hummels, ambaye atatimiza umri wa miaka 36 Desemba mwaka huu. (*Fabrizio Romano*)

**GRAVENBERCH ATAKIWA**

KLABU ya Galatasaray ya Ututruki inapanga kumnunua kiungo wa Liverpool, Mholanzi Ryan Gravenberch mwenye umri wa miaka 21, katika msimu wa joto. (*Fotomaki*)

**ZIRKZEE AWANIWA UNITED**

KLABU za Manchester United na Arsenal zinamwania mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 22, kutoka Bologna. (*Gazetta*)

**FERNANDEZ KUONDOKA**

MLINZI wa Real Madrid, Nacho Fernandez, ameamua kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, akitarajia kuhamia Ligi Kuu ya Soka ya Marekani. (*Marca*)

**NACHO AVUTIA JUVE**

MANCHESTER United, Juventus na Inter Milan pia ni ni baadhi ya klabu ambazo zinamvutia nahodha wa Real Madrid, Nacho Fernandez. (*Fichajes*)

**CARVALHO KUBAKI**

KIUNGO wa kati wa Ureno, Fabio Carvalho anatazamiwa kubaki na kupigania nafasi yake Liverpool msimu ujao chini ya kocha mpya wa klabu hiyo, licha ya kutakiwa na Hull City ambako mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, anacheza kwa mkopo. (*Football Insider*)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA ALALAMIKIA RATIBA NGUMU KWAO

**MANCHESTER,** England

### ●●● Siombi kitu maalum au upendeleo, nataka tu kuwalinda wachezaji wangu ni...

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amelalamikia ratiba ya Kombe la FA baada ya timu yake kutinga fainali kwa kuifunga Chelsea bao 1-0 Jumamosi, siku tatu baada ya kufungwa kwa mikwaju ya penalti na Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Bao la dakika za lala salama la Bernardo Silva liliwafanya City kutinga fainali, ingawa walipata bahati katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Chelsea, ambao waliadhibiwa kwa kutotumia nafasi nyingi walizotengeneza.

City, ambao hawakuwa na mshambuliaji wao, Erling Haaland, licha ya kufika fainali nyingine, Guardiola alikasirishwa wazi na timu yake kukosa muda wa kupona baada ya maumivu ya moyoni ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Jumatano.

"Haikubaliki kuturuhusu kucheza leo (juzi)," alisema Guardiola akiiambia BBC.

"Haiwezekani, kwa afya ya wachezaji. Si kawaida. Haikubaliki - dakika 120, hisia za Madrid, jinsi tunavyopoteza.

"Najua nchi hii ni maalum kwa Kombe la FA, lakini ni kwa ajili ya afya ya wachezaji. Sielewi jinsi tulivyonusurika."

Guardiola hakuweza kuelewa ni kwa nini mchezo wa City dhidi ya Chelsea haukupangwa Jumapili badala ya mechi ya nusu fainali ya Manchester United dhidi ya Coventry City ya daraja la pili, kwani hakuna klabu yoyote kati ya hizo iliyolazimika kucheza mechi katikati ya wiki.

**"Nguvu pekee niliyo nayo nasema hapa. Kwa nini tusingecheza Jumapili? Chelsea, Manchester United, Coventry hawakucheza katikati ya wiki," aliongeza Guardiola.**

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona na Bayern Munich pia alisifu kiwango cha wachezaji wake kwa kutafuta njia ya kushinda.

„Walichokifanya leo (juzi) ni mojawapo ya mambo makuu ambayo nimewahi kuona kutoka kwa kundi la wachezaji baada ya dakika 120 za soka siku ya Jumatano," alisema katika mkutano na wanahabari.

"Nataka tu kuwalinda wachezaji wangu. Ni akili ya kawaida. Siombi kitu maalum au upendeleo."

Msimamo wa Guardiola uliungwa mkono na kocha wa Arsenal, Mikel Arteta.

Arsenal, ambayo pia ilipoteza katika Ligi ya Mabingwa katikati ya juma, iliifunga Wolves 2-0 baadaye Jumamosi na kurejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, pointi moja juu ya City lakini ikiwa imecheza mechi moja zaidi.

"Si kuhusu sisi, Pep au mimi mwenyewe, ni juu ya ustawi wa wachezaji," alisema Arteta, msaidizi wa zamani wa Guardiola kule Man City.

"Unaposhiriki mashindano ya Ulaya kila timu inapaswa kushindana kwa njia sawa.

"Huwezi kuwa na timu ambayo haijacheza kwa siku saba, au siku tatu kabla, na ina muda zaidi wa kupona halafu lazima ucheze Ligi Kuu na Kombe la FA. Si sawa."

## HABARI MICHEZO



# TEN HAG AENDELEA KUMKOMALIA SANCHO

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amesisitiza hakuna kilichobadilika kwa Jadon Sancho ambaye aliondoka Manchester United baada ya kukataa kuomba radhi katika mgogoro wake na kocha huyo.

Sancho alirejea katika klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund kwa mkopo Januari, kutokana na mgogoro kati yake na Ten Hag.

Na, licha ya mfarakano huo, Sancho amerejesha kiwango chake nchini Ujerumani, na kuisaidia Dortmund hivi majuzi kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa.

Katika kipindi kigumu cha pili cha msimu kwa United, Ten Hag amekosolewa kwa kumruhusu Sancho kuondoka Old Trafford.

Akizungumza kabla ya mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Coventry City, Ten Hag alisema, „Tunajua Sancho ni mchezaji mzuri. Hilo si jambo la kushangaza.

„Ulikuwa mchezo mzuri sana - Dortmund dhidi ya Atletico Madrid. Uchezaji mzuri kutoka kwa Dortmund na kwa Jadon ni habari njema, alitoa mchango wake kwa matokeo ya Dortmund.

„Bila shaka, ninafuatilia soka la kimataifa na kuwafuatilia wachezaji walioko kwa mkopo katika klabu nyingine.“

Mustakabali wa muda mrefu wa Sancho ndani ya United si jambo pekee la kuzungumza Old Trafford, huku fununu pia zikimkumba kiungo wa Brazil, Casemiro.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, amekuwa akikabiliwa na majeraha ya mara kwa mara ya misuli ya paja, ambayo yanatatiza uwezo wake wa kucheza katika safu ya kiungo.

Hakika, kiwango cha uchezaji cha Casemiro msimu huu kimeshutumiwa sana, na amekuwa akihusishwa na kuwaniwa Saudi Pro League.

# Barca yataka saini ya Olmo

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeanzisha harakati za kumsajili Dani Olmo waliyemlenga kwa muda mrefu kutoka RB Leipzig, kwa mujibu wa ripoti kutoka Hispania.



Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alitumia miaka saba katika kikosi cha vijana cha Barcelona kabla ya kuhamia Dinamo Zagreb Julai 2014, alipokuwa na umri wa miaka 16 tu.

Olmo alikaa Croatia kwa miaka sita iliyofuata kabla ya kurejea RB Leipzig kwa mkataba wa miaka minne, lakini gazeti la Hispania Mundo Deportivo likiripoti kuwa Barcelona wanataka kumsajili tena, huku mawasiliano yakiwa tayari yameshafanywa na wawakilishi wa Mhispania huyo kuhusu uwezekano wa kurudi.

Man United na Bayern Munich inasemekana ‚kuvutiwa sana‘ na Olmo, ambaye amebakiza miaka mitatu kwenye mkataba wake kule Leipzig, lakini suala kubwa zaidi linaweza kuwa klabu hiyo ya Bundesliga kutokuwa tayari kumuuza mchezaji ambaye amechangia mabao nane na asisti tano msimu huu.

Barcelona huenda ikalazimika kuanzisha kipengele cha kutolewa kwa euro milioni 60 kilichoandikwa katika mkataba wa Olmo, na kuzunguka hitaji la Leipzig kutoa ruhusa ya kuhama.

Ikiwa Barcelona wanaweza kumudu dili kama hilo bado haijajulikana, ingawa mantiki inaweza kupendekeza kwamba wachezaji kadhaa watahitaji kuondoka kwa wababe hao wa Katalunya.

Frenkie de Jong amehusishwa na uhamisho wa fedha nyingi kwenda Bayern, kama vile mchezaji mwenzake Ronald Araujo - ambaye alizomewa na Ilkay Gundogan.

Pia kuna suala dogo la Barcelona kutaka kuwasajili Joao Felix na Joao Cancelo kwa mikataba ya kudumu kutoka Atletico Madrid na Manchester City.

# Alexander-Arnold: Liverpool inaweza kubeba ubingwa

**LIVERPOOL,** England

MCHEZAJI Trent Alexander-Arnold amekiri kuwa Liverpool inaweza kuwa imeipa Manchester City taji la Ligi ya England baada ya kuteleza hivi majuzi, lakini akasema unaweza kuwa wakati mzuri kwa klabu hiyo kurejea kwenye nafasi yao ya kuliwania taji hilo.

‚Wekundu‘ hao walipoteza kwa kushangaza wakiwa nyumbani kwa Crystal Palace Jumapili iliyopita, siku tatu baada ya kulazwa na Atalanta katika Uwanja wa Anfield kwenye Ligi ya Europa.



Liverpool walishindwa kuvuka upungufu katikati ya wiki, licha ya kushinda mechi ya marudiano na sasa wapo kwenye mbio za Ligi Kuu England.

Arsenal pia walipoteza pointi wikendi iliyopita na kuwapa Manchester City hatua ya kuwania taji.

Akizungumza na Sky Sports, Alexander-Arnold alikiri kwamba City ni ngumu sana kuwashinda katika mbio za ubingwa kwa sababu mara chache hufanya makosa, lakini akasema wachezaji wenzake wanalenga kudhibiti hatima yao wenyewe kwa kuchukua alama za juu kutokana na michezo sita waliyobakiza kucheza.

„Arsenal ilikumbana na hilo, tumepitia mara mbili au tatu, unapoingia kwenye mbio za ubingwa na Man City wanakuwa mstari wa mbele kabisa,“ alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.

„Huwezi kuteleza au kufanya makosa. Ukiwapa mkono wa juu huwa hawapepesi macho wakati huo. Hawaonekani kuwa wanyonge. Ni mashine iliyotiwa mafuta mengi.

„Hivyo ndivyo wanavyofanya, hakuna wa kuwazuia. Kuwapa faida hii kwa mechi sita kumalizika ni sawa na kuwapa ubingwa.

„Tumebakiza mechi sita, itasonga mbele. Lengo letu ni kushinda kila mchezo - hiyo ndiyo tu tunaweza na kujaribu. Itakuwa ngumu lakini nimeona katika wiki chache zilizopita za tofauti na asilimia.

„Ni timu nzuri sana ikiwa na kikosi walichonacho, ni vigumu kufikiria kwamba hawatashinda kwa wakati huu. Mambo ya ajabu yametokea kwenye Ligi Kuu.“

## HABARI MICHEZO

# NBC YAMTUZA AZIZ KI IKIFURAHIA KARIAKOO DABI NA WATEJA WAKE

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC Bank), ambayo ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania Bara, NBC Premier League, juzi ilinogesha shangwe za mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga kwa kuwapeleka Uwanja wa Benjamin Mkapa wateja wake ili kushuhudia mtanange huo ulioisha kwa timu ya Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-1, huku pia ilikabidhi zawadi kwa mchezaji wa washindi hao, Stephano Azizi Ki, ambaye aliibuka mchezaji bora wa ligi hiyo kwa mwezi Machi,

Zaidi, mdhanimini huyo aliandaa sehemu maalum za kutazama mechi hiyo (viewing points) kwenye baadhi ya mikoa hapa nchini ikiwamo Dar es Salaam, Arusha, Mwanza,Dodoma, Morogoro, Geita, Mtwara, Kigoma, Meru na Mbinga ili kutoa fursa kwa wapenzi wa mchezo huo ambao hawakuweza kufika uwanjani kufurahia mechi hiyo.

Jijini Dar es Salaam sehemu maalum zilizoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya kutazama mchezo huo ni Migahawa (Restaurants) za Samaki Samaki zilizopo maeneo ya Mlimani City na Masaki, pia Uvuvi Kempu pamoja na Hoppipola.

Wakizungumza kwenye hafla fupi ya chakula cha mchana na wateja wa benki hiyo kwenye Hoteli ya Hyatt the Kilimanjaro kabla ya kuwapeleka mashabiki hao uwanjani, Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Elvis Ndunguru, walisema hatua hiyo ni mwendelezo wa utaratibu wa benki hiyo kutumia mechi hizo maarufu kama 'Derby ya Kariakoo' kuandaa matukio kama hayo ili kutoa fursa kwao kufurahia ladha ya ligi hiyo inayoendelea kujiongezea umaarufu barani Afrika kutokana na udhamini mnono walioufanya.

"Umekuwa ni utaratibu wetu sasa kufurahia na wateja wetu kwenye kila mechi ya Ligi Kuu ya NBC kuanzia Dar es Salaam hadi mikoani kwa kutoa zawadi mbalimbali zikiwamo tiketi za bure kwa baadhi wateja kwa kuzingatia vigezo tofauti.

"Kwa kutambua uzito wa mechi hii huwa tunaitumia kama siku maalum kufurahia pamoja na wateja wetu kwa kuwaandalia chakula cha mchana, kutoa fursa kwa wao kufahamiana, kubadilishana mawazo yakiwamo ya kibiashara pamoja na kuwakumbusha kuhusu huduma zetu mbalimbali kisha pamoja tunaelekea uwanjani tukiwa kwenye msafara maalum kushuhudia pamoja mechi hiyo," alibainisha Ndunguru.

Zaidi Ndunguru aliongeza kuwa benki hiyo imejipanga zaidi kuendelea kuihudumia ligi hiyo kupitia huduma zake mbalimbali mahususi kwa timu zinazoshiriki ligi hiyo pamoja na Ligi Daraja la Kwanza (NBC Championship) na Ligi ya Vijana (NBC Youth League) ambazo zote zinadhaminiwa na benki hiyo.

"Kwenye hili tumejipanga kuhakikisha tunaendelea kutoa mikopo ya usafiri kwa timu zinazoshiriki Ligi Kuu kwa masharti nafuu, tunaendelea kutoa huduma za bima za afya kwa wachezaji na mabechi ya ufundi na mikopo mbalimbali kwa kuzingatia vigezo na masharti," aliongeza.

Mbali na matukio hayo pia wateja hao walipata fursa ya kupata huduma mbalimbali za kifedha kutoka NBC kupitia maofisa wa benki hiyo, ikiwamo kufungua akaunti pamoja na kufanya mihamala ya kifedha wakiwa maeneo hayo pamoja na viunga vya vya Uwanja wa Benjamin Mkapa.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru (kushoto) akikabidhi tuzo kwa mchezaji wa Yanga, Stephano Aziz Ki, aliyetangazwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania Bara kwa mwezi wa Machi. Makabidhiano hayo yalifanyika mapema kabla ya mchezo wa Ligi Kuu ya NBC kati ya Yanga na Simba uliopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-1. **MPIGAPICHA WETU**

## CECAFA Chalenji yapigwa kalenda

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MASHINDANO ya CECAFA Senior Chalenji ambayo kwa mwaka huu yatafanyika hapa Visiwani Zanzibar, yamesogezwa mbele hadi Julai 6, badala ya Juni 29, tarehe iliyopangwa hapo awali.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Hussein Ahmada Vuai, akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, alisema kusogezwa mbele kwa mashindano hayo kumetokana na sababu ambazo zipo nje ya uwezo wao, ikiwamo ombi la wadhamini ambao wameomba kufanyika mwezi huo.

Alisema matarajio yao katika mashindano hayo ni kuwapo kwa ushindani mkali kwa nchi shiriki, ambapo sasa yataanza Julai 6 hadi 21, mwaka huu.

Vuai alisema maandalizi yanakwenda vizuri na tayari timu ya CECAFA ambayo walikuwa na ukaguzi wa miundombinu kwa ujumla wake kwa ajili ya mashindano ya shule kwa vijana walipata nafasi hiyo ya kukagua miundombinu yote ya Zanzibar kwa hatua ya awali.

Aidha, alisema timu hiyo ya ukaguzi, inatarajiwa kuja tena kufanya ukaguzi huo kutokana na taratibu zao, ingawa wameridhishwa na hali ya miundombinu ya hapa nchini.

"Wazanzibari wajiandae mashindano yapo na tunatarajia ukaguzi wa awamu ya pili ambao ndio wa mwisho utakaofanyika ndani ya mwezi ujao, lakini tunaamini kila kitu kinakwenda vizuri," alisema.

Hata hivyo, alisema mpaka sasa wamekuwa na ushirikiano mzuri na wanajiandaa vema kuhakikisha mashindano hayo yanafanikiwa.

## *Simba, Yanga rekodi kibao*

INATOKA UKURASA 24

Matokeo ya mechi hiyo yameifanya Yanga kuukaribia ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo ikiwa imefikisha pointi 58, ikicheza mechi 22 na kusalia na michezo minane ikiendelea kujichimbia kileleni mwa msimamo Ligi Kuu, huku Simba iliyocheza michezo 21 mpaka sasa, ikisalia na pointi zake 46, ikiwa nafasi ya tatu, ikibakisha michezo tisa kabla ya kuhitimisha mechi zake za msimu huu.

## Gamondi asisitiza...

INATOKA UK. 24

chezo takriban saba iliyopo mbele yao na anaamini ni migumu kuliko ambayo wametoka kucheza.

"Hatuna uhakika kwa asilimia zote kwa sababu tuna mechi za ushindani, tunacheza Jumamosi nyumbani halafu tunaenda kucheza ugenini, tunahitaji kupata pointi muhimu katika hizo mechi ili kufikia malengo yetu," alisema Gamondi

Mshambuliaji wa Yanga, Joseph Guede alisema anafurahi kufunga bao la ushindi katika mchezo huo wa Derby, jambo ambalo linampa mwanga wa kuendelea kufanya hivyo kila anapopata nafasi.

Naye Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola, alisema mechi ilikuwa nzuri na ngumu kipindi cha kwanza dakika 10, waliweza kutengeneza nafasi mbili, shida lakini bado iko palepale.

"Bado tatizo letu halijapata majibu tumetengeneza nafasi, lakini kuzigeuza kuwa mabao ni ngumu, pia tulilazimika kufanya mabadiliko ya lazima baada ya Henock Inonga kuumia na mchezaji aliyekuja kuchukuwa nafasi yake akasababisha penalti na kuwapinzani kupata bao la kwanza.

"Kuhusu ubingwa ni ngumu sana, lakini bado tunatakiwa kupambana kushinda katika mechi zilizosalia. Baada ya kuwa nyuma ya bao mbili tulilazimika kuongeza watu mbele ili kuweza kupata bao na kufanikiwa kufunga moja," alisema Matola.

Na kuhusu safu ya ulinzi alisema bado wamekuwa wakiruhusu bao katika kila mechi jambo ambalo wataendelea kulifanyia kazi katika sehemu zote za mapungufu wakiandaa na michezo iliyosalia.

Michezo
Jumatatu Aprili 22, 2024
Nipashe



Guardiola alalamikia ratiba ngumu UK. 21

JUU KWA JUU...



Wachezaji wa Simba na Yanga wakiwania mpira wa juu katika mechi ya 'Dabi' ya Kariakoo iliyopigwa juzi Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Yanga ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Gamondi asisitiza ubingwa bado

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuchora ramani nzuri ya kutwaa taji la ubingwa kwa msimu huu, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameendelea kusisitiza kuwa wanahitaji kupambana na kujitoa katika michezo iliyosalia ya mzunguko huu wa lala salama Ligi Kuu Tanzania Bara ili kufikia malengo hayo.

Amesema anaimani wametoka kwenye michezo migumu, lakini anaamini wanapoelekea ni zaidi ya walipotoka hasa katika michezo saba iliyosalia ya Ligi hiyo kuhakikisha wanavuna pointi muhimu katika kila mchezo uliopo mbele yao.

Gamondi alisema hayo juzi baada ya kukamilika kwa dakika 90 za mchezo wa Kariakoo ,Derby' kwa kufanikiwa kuvuna pointi tatu zingine mbele ya watani wao wa jadi, Simba kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2 -1, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Alipongeza utendaji kazi mzuri wa kundi lake la wachezaji kwa tabia ya kupambania timu.

"Mambo muhimu zaidi ni kucheza ndani ya uwanja, bila shaka tumefanikiwa mipango yetu, najivunia wachezaji wangu maana hata kwa nyakati ambazo hawachezi vizuri, lakini wanapambana kupata matokeo mazuri," alisema Kocha huyo.

Aliongeza kuwa haikuwa mechi rahisi, lakini anajivunia kiwango cha wachezaji wake katika kila mechi ikiwamo hiyo ya Derby kwa kucheza kwa tahadhari na kuwaheshimu wapinzani wao, hivyo kufanikiwa kuvuna pointi tatu zingine.

Kuhusu ubingwa, alisema licha ya kupata mwanga nzuri, lakini hawajihakikishii kwa sababu bado wana mi-

INAENDELEA UK. 23

# Simba, Yanga rekodi zatawala Dabi

## ●●● Mguu wa kushoto wanogesha mchezo kwa timu zote, huku Aziz Ki akizidi...

**Na Adam Fungamwango**

MECHI ya watani wa jadi, iliyochezwa juzi, Uwanja wa Benjamin Mkapa, iliyomalizika kwa Yanga kuifunga Simba mabao 2-1, imeacha rekodi kadhaa ikiwamo mabao yote matatu kufungwa kwa mguu wa kushoto.

Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mzunguko wa pili, mabao yote yalifungwa katika lango la Kusini na wachezaji wa kigeni watupu, huku Waivory Coast wawili, Joseph Guede wa Yanga na Freddy Michael, waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo, wakiweka rekodi ya kufunga mabao katika dabi zao za kwanza nchini.

Kiungo mshambuliaji wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, aliingia kwenye rekodi ya kufunga mabao kwenye mechi zote mbili za msimu mmoja, akiifikia rekodi ya Amissi Tambwe aliyefanya hivyo msimu wa 2015/16.

Alifunga bao moja katika mechi ya mzunguko wa kwanza, Novemba 5, mwaka jana, kwenye uwanja huo huo, akiongoza timu yake kushinda mabao 5-1.

**Aziz Ki, pia ameendeleza rekodi yake nzuri ya kuifunga Simba, kwani hata msimu uliopita alifanya hivyo katika mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu katika mchezo wa dabi uliochezwa, Oktoba 23, 2022, na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1, kabla ya Simba kuifunga Yanga mabao 2-0 katika mechi ya mzunguko wa pili iliyochezwa Aprili 16, 2023.**

Baada ya yeye mwenyewe kufanyiwa madhambi na Hussein Kazi ndani ya eneo la hatari, Aziz Ki, raia wa Burkina Faso alifunga bao hilo kwa kutumia mguu wa kushoto dakika ya 19, kabla ya Guede kupachika la pili dakika ya 37, alipopokea mpira mrefu uliopigwa kutoka katikati ya uwanja, akaumiliki peke yake mabeki wa Simba wakidhania kuwa ameotea, akamlamba chenga kipa Lakred kabla ya kuujaza wavuni.

Freddy alipachika bao la kufutia machozi kwa mguu wa kushoto dakika ya 73, akiitendea haki pasi ya Clatous Chama, akiwalambisha sakafu, Ibrahim Hamad ,Bacca' na Bakari Mwamnyeto, kabla ya kuukwamisha wavuni.

Mechi ya juzi imemfanya Aziz Ki, kuendelea kuongeza pengo la ufungaji katika Ligi Kuu baina yake na Feisal Salum wa Azam FC, akifikisha mabao 15, Freddy akifikisha manne, na Guede matatu.

Yanga imerudia rekodi yake iliyoiweka msimu wa 2015/16 kuifunga Simba mara mbili kwa msimu mmoja, ambapo ilikuwa mara ya mwisho kwa mechi za dabi timu moja kushinda mara hizo kwa msimu mmoja.

Mechi ya mzunguko wa kwanza ilishinda mabao 2-0, yaliyowekwa wavuni na Amissi Tambwe na Malimi Busungu na mzunguko wa pili ilishinda idadi hiyo hiyo ya mabao yaliyofungwa na Donald Ngoma na Tambwe.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >